Ushindani wa Kodi Afrika ya Mashariki

Mbio za kuelekea chini?

Motisha ya Kodi na Upotevu wa Mapato Tanzania

Ushindani wa Kodi Afrika ya Mashariki

Mbio za kuelekea chini?

Motisha ya Kodi na Upotevu wa Mapato Tanzania

Tax Justice Network -Africa
Chania Avenue, Kilimani
P.O.Box 25112, Nairobi 00100 Kenya
Tel. +254 20 247 3373
infoafrica@taxjustice.net

ActionAid International
Postnet Suite 248
Private bag X31
Saxonwold 2132
Johannesburg, South Africa
www.actionaid.org

Policy Forum
Plot 14, Sembeti Road
Off Old Bagamoyo Road, Mikocheni B.
P.O. Box 38486
Tel. +255 22 2780200
www.policyforum.or.tz

Chapisho hili limetolewa kwa pamoja na Mtandao wa Tax Justice Network–Africa na Shirika la Kimataifa la ActionAid (ActionAid International) na kutafsiriwa na Policy Forum.

Tunatoa shukurani zetu kwa wafuatao kwa mchango wao katika utayarishaji wa Taarifa hii: Mark Curtis, Lucy Kambuni, James Daniels, Alvin Mosioma, Vera Mshana, Soren Ambrose, Frances Ellery, na Dr. Honest Prosper Ngowi.

Kuhusu TJN-A

Mtandao wa *Tax Justice Network –Africa-TJN-A* ulianzishwa mwaka 2007 kama juhudi za kiafrika kuchechemua kuhusu mfumo wa kodi uliyowa haki kwa jamii kidemokrasia na maendeleo katika Afrikana pia ni mwanachama wa Global Tax Justice Network. TJN-A hutetea mfumo wa kodi unaojali wenye kipato duni na kuimarisha mfumo wa kodi unaohimiza makusanyo toka rasilimali za ndani . TJN-A ina lengo la kutoa changamoto kwa sera za kodi zenye madhara na mifumo inayopendelea matajiri na kuendeleza hali zisizo sawa katika jamii.

Kuhusu ActionAid

Shirika la Kimataifa la ActionAid (ActionAid International -AAI) ni shirika lisilo la kisiasa wala la kidini ni la kimaendeleo ambalo limekuwa likifanya kazi nchini Kenya tangu mwaka 1972. ActionAid huwezesha michakato ya kuondoa umaskini na kuhakikisha jamii zinapata haki zao kwa kupitia miradi ya kuondoa umaskini, kujenga uwezo wa taasisi na kuimarisha ushawishi wa sera za jamii. Kimsingi shirika limejikita katika kuendeleza na kulinda haki za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kiraia na kisiasa, na inategemeza miradi na mipango inayonufaisha watu wenye kipato duni na walio pembezoni.

Kuhusu Policy Forum

Policy Forum ni mtandao wa Asasi zaidi ya 100 za kiraia za Tanzania zilizoungana kwa pamoja kwa dhamira ya kushawishi michakato ya uundwaji sera ili kupunguza umaskini, kuleta usawa na demokrasia wakijikita zaidi katika uwajibikaji wa serikali kwa matumizi ya fedha za umma.

Tunapenda kutambua Taasisi zifuatazo kwa msaada wa kifedha katika uchapishaji wa utafiti huu: Oxfam, Novib, Trust Africa, Shirika la Kimaendeleo la Ki-Norwegian (Norwegian Agency for Development Cooperation (NORAD) and Christian Aid. Wawajibikaji pekee kwa yaliyomo katika chapisho hili ni TJN-A,Policy forum na Action Aid International (AAI), na hayana uhusiano wowote na Taasisi zilizofadhili uchapishaji.

Muhtasari

Serikali ya Tanzania inatoa wigo mpana wa motisha wa kodi kwa wafanya biashara ili kuvutia viwango vikubwa zaidi vya uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDIs) nchini.

Utoaji wa motisha ya kodi Tanzania, tunaweza kusema ni sehemu ya ushindani wa kodi miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika ya Mashariki (EAC). Kufuatia uundaji wa EAC mwaka 1999, Kenya, Tanzania, na Uganda walianzisha umoja wa forodha (eneo ambalo halina ushuru wa forodha na lenye kiwango cha tozo ya bidhaa zinazotoka nje ya nchi kinachofanana) mwaka 2005, na Rwanda na Burundi wakajiunga mwaka 2009. Hali hii imejenga eneo pana zaidi kikanda kwa uwekezaji wa moja kwa moja toka nje (FDIs) kwa ujumla hususan kwa uwekezaji-utafutaji masoko.[1] Chini ya soko la pamoja la Jumuia ya Afrika ya Mashariki, mashirika ya kibiashara kwa ujumla na hasa mashirika ya biashara za kimataifa yanayojihusisha na uwekezaji wa nje yanaweza kuwekeza popote ndani ya nchi wanachama. Wakati huo huo lakini, nchi zinashawishika kuongeza motisha ya kodi kuvutia uwekezaji wa nje endelevu ili kunufaika kutokana na huu uwekezaji kwa njia ya ajira, mapato kutokana na kodi, ada, mrabaha na gawio kati ya nyinginezo; mfungamano wa kisekta; uhamishaji wa kiteknolojia, na faida nyingine zinazowezekana kutoka kwa wawekezaji wa nje kwa uchumi wa nchi wanazowekeza. Uchambuzi wetu unaonesha kuwa utoaji wa motisha ya kodi katika Kanda ya Afrika ya Mashariki kwa ujumla na hasa nchini Tanzania unaonesha ushindani wa kodi wenye madhara na unaweza kuwa 'mbio za kuelekea chini'.

Tanzania hutoa wigo mpana wa motisha wa kodi. Katika Kanda za Usindikaji wa Bidhaa kwa Mauzo Nje ya Nchi (EPZs) na Kanda Maalum za Kiuchumi (SEZs), makampuni yanasamehewa kulipa kodi ya mapato ya shirika na kodi zote na ada zinazodaiwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGAs), na pia hupewa msamaha wa ushuru wa kuingiza mali ghafi na zana za uzalishaji viwandani. Kama wanauza nje ya nchi kiwango kisichopungua asilimia 80 ya bidhaa zao, bidhaa hizo hazitozwi kodi. Makampuni ya uchimbaji wa madini yanapewa upendeleo maalum: hayalipi ushuru wa mafuta, yana msamaha wa kodi ya faida ya kimtaji. Yanalipa kiwango

1 Uwekezaji wa nje unaweza kuwa : Utafutaji wa masoko; utafutaji wa rasilimali; utafutaji wa ufanisi

kidogo cha ushuru wa stempu na hupata unafuu wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT). Vikundi vingine vya wawekezaji wanaonufaika kutokana na motisha ni pamoja na makampuni yenye vyeti vya motisha toka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC); wawekezaji wenye hadhi ya "Uwekezaji Nyeti" na wawekezaji katika sekta ya kilimo.

Uchambuzi unaonesha kuwa wanaonufaika na motisha na misamaha ya kodi ni kundi dogo la wawekezaji kutoka nje, wakati wanaoathirika kutokana na upotevu mkubwa wa mapato ni wakazi na nchi kwa ujumla. Hata hivyo, taarifa ya mwaka 2006 ya Idara ya Afrika ya Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) kuhusu Afrika ya Mashariki, inaonesha kuwa " Motisha ya uwekezaji – hususan motisha za kodi – siyo jambo la msingi katika kuvutia uwekezaji wa nje" Mambo ya msingi zaidi ni miundo mbinu imara, gharama ndogo za utawala katika uanzishaji na uendeshaji wa biashara, utulivu wa kisiasa, na sera ya uchumi mkuu inayotabirika. Katika Tanzania, uanzishaji wa kanda za usindikaji wa bidhaa kwa mauzo nchi za nje (EPZs) mwaka 2002 "haikuleta matokeo bayana katika ongezeko la uwekezaji wa nje" taarifa ya Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) imeainisha. Uganda imeendelea kuvutia kiwango kikubwa cha uwekezaji wa moja kwa moja wa nje (FDIs) kuliko Tanzania, ambayo hutoa motisha kubwa na nzuri zaidi kwa uwekezaji.

Serikali inatambua kuwa misamaha ya kodi na motisha huambatana na upotevu mkubwa wa mapato na inachukua hatua kadhaa za kupunguza. Hata hivyo, maendeleo ni ya mwendo pole na hali halisi ya uwajibikaji wa serikali inatatanisha. Cha muhimu zaidi katika uchambuzi huu, ni kwamba haieleweki hatua zaidi ambazo serikali itachukua kupunguza motisha ya kodi inayotolewa kwa makampuni ya uchimbaji wa madini, biashara zinazoendeshwa katika kanda za usindikaji wa bidhaa kwa mauzo ya nje (EPZs) na kanda maalum za kiuchumi (SEZs); wawekezaji wenye vyeti vya kituo cha uwekezaji Tanzania vilevile na wale wenye hadhi ya "wawekezaji nyeti'.

Kwa maoni yetu, serikali inapaswa:

- Kuondoa baadhi ya motisha za kodi zinazotolewa ili kuvutia na kubakisha uwekezaji wa moja kwa moja wa nje (FDIs), hasa wale walio katika sekta za madini, kanda za usindikaji wa bidhaa kwa mauzo ya nje (EPZs) na kanda maalum za kiuchumi (SEZs)
- Kufanya marejeo yatakayoweka wazi kwa umma motisha zote za kodi kwa lengo la kupunguza au kuondoa nyingi katika hizo, hasa zile

zinazohusu madaraka yaliyokasimiwa kwa Mawaziri

- Kutoa kila mwaka, wakati wa uandaaji wa bajeti mchanganuo wa bajeti utakaowekwa wazi kwa umma, unaoonesha gharama serikali inayoingia kutokana na motisha ya kodi na wanaonufaika kutokana na matumizi ya kodi hiyo.
- Kuchukua dhamana na kuwajibika kwa umma katika mambo yote yanahusu utoaji wa motisha na misamaha
- Kuchukua hatua zaidi za kukuza na kuratibu juhudi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) kukabiliana na ushindani wa kodi wenye madhara na kuunga mkono juhudi za sasa za kuzitaka makampuni ya kimataifa kutoa taarifa juu ya shughuli zao katika nchi kwa kila nchi.
- Kuchukua hatua mahususi za usimamizi wa kifedha na kisera ili kuzuia uhamishaji usiyo halali wa fedha haramu wa faida zinazotokana na motisha kubwa za ki- kodi na zisizo za kikodi zinazotolewa na serikali.

Vifupisho

AfDB	Benki ya Maendeleo ya Kiafrika *(African Development Bank)*
CAG	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu *(Controller and Auditor General)*
DFP	Miradi Inayogharimiwa na Wahisani *(Donor Funded Projects)*
DSE	Soko la Mitaji la Dar es Salaam *(Dar Es Salaam Stock Exchange)*
EAC	Jumuiya ya Afrika Mashariki *(East African Community)*
EPZs	Kanda za Usindikaji Bidhaa kwa Mauzo ya Nje *(Export Processing Zones)*
EPZA	Mamlaka ya Kanda za Usindikaji Bidhaa kwa Mauzo ya Nje *(Export Processing Zones Authority)*
EU	Jumuiya ya Ulaya *(European Union)*
FDI	Uwekezaji wa Moja kwa Moja wa Nje *(Foreign Direct Investments)*
GDP	Zao Ghafi la Ndani (Gross Domestic Product)
IMF	Mfuko wa Fedha wa Kimataifa *(International Monetary Fund)*
LGAs	Mamlaka ya Serikali za Mitaa *(Local Government Authorities)*
MNEs	Makampuni Mtandao ya Biashara ya Kimataifa *(Multinational Enterprises)*
NGO	Asasi Zisizo za Kiserikali *(Non Governmental Organization)*
PAYE	Lipa Kadri Unavyopata *(Pay As You Earn)*
TMAA	Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania *(Tanzania Minerals Audit Agency)*
TRA	Mamlaka ya Mapato Tanzania *(Tanzania Revenue Authority)*
Tshs	Shilingi ya Tanzania *(Tanzanian Shillings)*
UN	Umoja wa Kimataifa *(United Nations)*
USD	Dola ya Marekani *(United States of America Dollar)*
SEZs	Kanda Maalum za Kiuchumi *(Special Economic Zones)*
VAT	Kodi ya Ongezeko la Thamani *(Value Added Tax)*

Yaliyomo

Muhtasari vi

Vifupisho ix

Utangulizi 1

1. Motisha ya Kodi Tanzania 5
2. Wanaonufaika na Kupoteza Kutokana na Motisha wa Kodi 12
3. Matatizo ya Motisha wa Kodi 28
4. Sera ya Serikali Kuhusu Motisha ya Kodi 37
5. Mapendekezo 40

Marejeo 42

Utangulizi

Serikali ya Tanzania inatoa wigo mpana wa motisha kwa ujumla na hasa motisha ya kodi. Madhumuni ni kuvutia Uwekezaji wa nje (FDIs) nchini kwa kiwango kikubwa na endelevu. Uwepo wa misamaha ya kodi umefanya mashirika mengi hususan makampuni ya madini, uzalishaji wa bidhaa za viwandani, mahoteli na loji za watalii, kukwepa kulipa kodi kabisa[2]. Utafiti huu unaonesha kuwa motisha hizi za kodi zinapelekea upotevu mkubwa wa mapato na si lazima kuvutia na kuendeleza uwepo wa uwekezaji wa moja kwa moja wa nje (FDIs).

Makisio mbalimbali yapo yanayoonesha upotevu wa mapato unaotokana na Serikali kutoa motisha na misamaha ya kodi. Tunaonesha kuwa, kwa kuzingatia haya makisio mbalimbali, upotevu wa mapato kutokana na *misamaha yote na motisha ya kodi* yanaweza kuwa juu kufikia kiasi cha shilingi za Tanzania trilioni 1.8 (dola za kimarekani bilioni 1.23) mwaka 2008 na ya kwamba *kiwango cha chini kabisa* cha upotevu wa mapato unaotokana na *motisha ya kodi* zinazotolewa kwa makampuni peke yake inakaribia shilingi za Tanzania bilioni 381(dola za kimarekani milioni 174) kwa mwaka (kwa miaka ya 2008/9 – 2009/10). Kwa mwaka 2010/11 misamaha ilifikia kiasi cha shilingi 1,016,320,300,000 ambayo ni kama asilimia 18 ya makusanyo yote ya kodi. Hili ni ongezeko la asilimia 3 ya kiwango cha misamaha ikilinganishwa na jumla ya makusanyo ya mapato katika mwaka wa fedha 2009/10 ambayo ilikuwa asilimia 15.[3]

Kutokana na misamaha, nchi inanyimwa rasilimali fedha zinazohitajika sana kwa ajili ya matumizi ya umma ya gharama za bidhaa na huduma kwa bajeti zote mbili, ya maendeleo na ya matumizi ya kawaida. Hizi ni rasilimali ambazo zikikusanywa zitasaidia sana katika kupunguza idadi ya asilimia 36 ya Watanzania wanaoishi chini ya mstari wa umaskini. Kwa mfano, kama mapato ya taifa yanayopotea kutokana na misamaha ya kodi yangelitumika kuboresha elimu na afya, bajeti ya elimu ingeongezeka kwa zaidi ya 1 ya 5 na bajeti ya afya ingeongezeka kwa zaidi ya 2 ya 5. Jambo hili ni muhimu wakati wastani wa pato kwa mtu ni dola za kimarekani 530 tu, na theluthi moja ya wakazi milioni 44 wanaishi chini ya mstari wa umaskini.

2 Odd-Helge Fjeldstad and Kari Heggstad, 'Tax system in Tanzania: Capacity and Constraints', *The Citizen*, 26 June 2011

3 Tazama Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu (CAG Report) ya 2011

Mwaka 2009/10 Tanzania ilikusanya Shilingi za Tanzania trilioni 4.45 kwa kodi zote. Kati ya hizi kama asilimia 30 zilitokana na kodi ya ongezeko la thamani (VAT), kodi ya mapato na ushuru wa uingizaji wa bidhaa.[4] Kodi zilizokusanywa zilifikia kiasi cha asilimia 14.6 ya Zao Ghafi la Ndani (GDP)[5]kwa mwaka 2009/10, hata hivyo Mfuko wa Fedha wa Kimataifa unakisia kwamba Tanzania ina uwezo wa kupata mapato yanayotokana na kodi kwa kiwango cha asilimia 20.9 ya Zao Ghafi la Ndani (GDP)[6]. Hii ina maana kwamba pengo lake la kodi – tofauti kati ya makusanyo halisi na uwezo uliopo wa makusanyo ya mapato – ilikuwa kubwa kwa kiwango cha asilimia 6.3 ya Zao Ghafi la Ndani kwa mwaka 2009/10, inayofikia kiasi cha shilingi za Tanzania trilioni 1.9.[7]

Kumekuwepo na ongezeko katika kiwango cha misamaha kama asilimia ya jumla ya makusanyo ya kodi nchini Tanzania. Hali hii inaoneshwa katika jedwali lililopo hapa chini.

Jedwali 1: Makusanyo na Misamaha ya Kodi kwa 2009/10 na 2010/11

Maelezo	**2010/2011**	**2009/2010**
Makusanyo halisi	5,550,205,244,378	4,637,686,999,618
Misamaha	1,016,320,300,000	680,667,900,000
Uwiano wa misamaha na makusanyo halisi	18%	15%
Mapungufu katika makusanyo	298,888,455,622	391,235,100,382
Ziada kama misamaha isingetolewa	717,431,844,378	289,432,799,618

Chanzo: Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu 2010/2011

4 MOF, Financial Statement and Revenue Estimates, 2011/12 Budget, Vote 21, www.mof.go.tz.

5 IMF, *Staff Report for the 2011 Article IV Consultation and Second Review under the Policy Support*

6 IMF, *Seventh Review under the Policy Support Instrument*, 18 May 2010, p.20

7 IMF, *Staff Report for the 2011 Article IV Consultation and Second Review under the Policy Support Instrument*, 21 April 2011, p.25; Pengo katika kodi katika shilingi ya Tanzania inatokana na Zao ghafi la ndani (GDP) ya shilingi ya Tanzania bilioni 30,321 billioni mwaka 2009/10

Utoaji wa motisha ya kodi nchini Tanzania inaweza kuwa ni sehemu ya ushindani wa kodi miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC). Kufuatia uundaji wa EAC mwaka 1999, Kenya, Tanzania, na Uganda waliunda umoja wa forodha (Kufuatia uundaji wa EAC mwaka 1999, Kenya, Tanzania, na Uganda walianzisha umoja wa forodha (eneo ambalo halina ushuru wa forodha yenye kiwango cha tozo ya bidhaa zinazotoka nje ya nchi kinachofanana) mwaka 2005, na Rwanda na Burundi wakajiunga nao mwaka 2009. Hali hii imejenga eneo pana zaidi kikanda kwa Uwekezaji wa moja kwa moja (FDIs) toka nje kwa ujumla hususan kwa uwekezaji-utafutaji masoko.[8] Chini ya soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, mashirika ya kibiashara kwa ujumla na hasa mashirika ya biashara za kimataifa yanayojihusisha na uwekezaji wa nje yanaweza kuwekeza popote ndani ya nchi wanachama. Wakati huo huo lakini, nchi zinashawishika kuongeza motisha ya kodi kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja wa nje endelevu (FDIs) ili kunufaika kutokana na huu uwekezaji kwa njia ya ajira, mapato kutokana na kodi, ada, mrabaha na gawio kati ya nyinginezo; mfungamano wa kisekta; uhamishaji wa kiteknolojia, na faida nyingine zinazowezekana kutoka kwa wawekezaji wa nje kwa uchumi wa nchi wanazowekeza. Uchambuzi wetu unaonesha kuwa utoaji wa motisha wa kodi katika Kanda ya Afrika Mashariki kwa ujumla na hasa nchini Tanzania unaonesha ushindani wa kodi wenye madhara na unaweza kuwa "mbio za kuelekea chini".

Kwa bahati mbaya nchi zinazidi kushawishiwa kuongeza motisha ya uwekezaji kwa ujumla hususan motisha za kodi ili kuvutia na kudumisha zaidi uwekezaji wa moja kwa moja toka nje (FDIs); kama inavyobainishwa katika taarifa ya Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) ya mwaka 2006:

"Ongezeko la Ushindani wa Uwekezaji wa moja kwa moja toka nje (FDIs) na ukuaji wa shinikizo la kutoa misamaha ya kodi na motisha zingine za uwekezaji ili kuvutia (na kudumisha) wawekezaji kunaweza kupelekea hali ya "mbio za kuelekea chini," hali ambayo itaathiri wote watatu, (yaani Kenya, Uganda na Tanzania) nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC). Usipodhibitiwa ushindani huu utapelekea katika upotevu wa mapato, hasa kwa Tanzania na Uganda, na kutishia lengo la kuboresha makusanyo ya mapato[9]

8 Uwekezaji wa nje unaweza kuwa : Utafutaji wa masoko; utafutaji wa rasilimali; utafutaji wa ufanisi

9 IMF, *Kenya, Uganda and United Republic of Tanzania: Selected Issues*, 1 December 2006, p.5

Uchambuzi wetu unadokeza kwamba hali hii ndiyo hasa inayojitokeza na kwamba wigo mpana wa motisha za kodi unaotolewa na Tanzania na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unawaongoza kwenye "mbio za kuelekea chini"

Kisanduku 1: Kuelewa Motisha ya Kodi

Motisha ya kodi inatafsiriwa kama "punguzo, kuachwa au msamaha wa kodi inayotakiwa kulipwa, inatolewa kama kivutio ili kuingia katika shughuli maalum kama vile uwekezaji katika bidhaa mtaji kwa muda maalum.[10] Motisha ya kodi ni mfumo wa kifedha wa motisha ya uwekezaji na inajumuisha likizo ya kodi ya mapato kwa mashirika makubwa na punguzo la kiwango cha kodi ya mapato. Motisha zisizo za kifedha au zisizo za kodi zinajumuisha ruzuku za moja kwa moja kama vile ruzuku ya serikali, mikopo na dhamana kwa miradi lengwa. Motisha ya kodi hutolewa ili kuvutia "Uwekezaji wa moja kwa moja wa kutoka Nje ya nchi (FDI)" na/au kuendeleza sera maalum za kiuchumi, kama vile kuvutia uwekezaji katika sekta fulani fulani.

Motisha ya Uwekezaji[11]

Motisha ya Kodi ya Mapato kwa Mashirika Makubwa

- Likizo ya kodi au punguzo la viwango vya kodi
- Mikopo ya kodi
- Posho ya uwekezaji
- Uchakavu wa kasi
- Posho ya kuwekeza tena au ya upanuzi

Motisha zingine za kodi

- Msamaha au punguzo la zuio la kodi
- Msamaha wa tozo la uingizaji bidhaa toka nje
- Msamaha wa ushuru wa upelekaji bidhaa nje ya nchi
- Msamaha wa kodi za mauzo, malipo ya vibarua au umiliki wa mali
- Punguzo la uchangiaji katika mifuko ya uhifadhi wa jamii

Motisha za Kifedha na Usimamizi

- Ruzuku au Misaada ya kifedha
- Ruzuku au udhamini wa mikopo
- Utoaji wa miundombinu, mafunzo
- Upendeleo katika kupata tenda za serikali
- Kulindwa dhidi ya ushindani wa uingizaji bidhaa nchini
- Ruzuku katika gharama za upokeaji wa bidhaa na huduma
- Kupunguza sheria za udhibiti wa viwango vinavyotakiwa

10 Tazama *http://www.businessdictionary.com/definition/tax-incentive.html* ya tarehe 11th April, 2011.

11 IMF, Kenya, Uganda and United Republic of Tanzania: Selected Issues, 1 December 2006, p.10

6. Motisha ya Kodi Tanzania

Tanzania hutumia wigo mpana wa motisha za kodi. Baadhi ya hizi zinaoneshwa kama ifuatavyo:

Motisha za kodi kwa wote wenye cheti cha motisha kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)[12]

Wawekezaji wanaofikia kiwango cha chini cha uwekezaji cha dola za kimarekani 100,000 kwa makampuni ya ndani, na dola za kimarekani 300,000 kwa makampuni ya kigeni, wanastahili kupewa cheti cha motisha inayotolewa na TIC. Wenye vyeti hivyo wanapata:

- Msamaha wa ushuru wa uingizaji bidhaa za mtaji wa mradi katika sekta muhimu zikiwa ni pamoja na kilimo, madini na miundombinu
- Msamaha wa asilimia 5 wa ushuru wa uingizaji wa bidhaa za mtaji wa mradi katika sekta za kipaumbele zikijumuisha usafiri wa anga, majengo ya biashara, uendelezaji wa biashara, benki zinazotoa mikopo midogo midogo kwa ajili ya wafanya biashara ndogo ndogo, viwanda, maliasili na samaki, radio na matangazo ya luninga na utalii.
- Asilimia 100 ya ruzuku mtaji (punguzo la kodi kutokana na matumizi yatokanayo na mtaji) kwa mitambo ya viwandani, majengo, mashine za viwandani na matumizi ya kilimo.
- Asilimia 0 ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) katika malighafi za uchimbaji wa madini, matumizi ya kilimo, utalii, na bidhaa za viwandani kwa mauzo nje ya nchi
- Chini ya mpango wa ushuru wa bidhaa zinaoingia ndani ya nchi, miradi ya biashara zina kibali cha kurejeshewa ushuru uliolipwa kwa malighafi zinazoingia ndani ya nchi kwa lengo la mauzo nje ya nchi au zitakazouzwa kwa mashirika ya kimataifa kama vile Umoja wa Kimataifa(UN)
- Miradi ya biashara inaweza kubeba hasara kwa miaka mitano dhidi ya faida za baadaye,

12 Tazama 'Corporate Tanzania: Business, Trade and Investment Guide 2010/2011', *www.corporate-tanzania.com*, p.57; Tanzania Investment Centre, 'FAQ Related to Investing in Tanzania' *http://www.tic.co.tz/*

Motisha za kodi kwa wawekezaji kwenye kanda za bidhaa zinazotayarishwa kwa mauzo ya nje (EPZs) na kanda maalum za kiuchumi (SEZs)[13]

Kanda za utayarishaji wa bidhaa kwa mauzo ya nje za Tanzania ziliundwa kwa mujibu wa Muswada wa sheria ya mwaka 2002 na ulilenga kuvutia Uwekezaji wa nje wa moja kwa moja (FDIs) na hivyo kukuza uuzaji wa nje, kuongeza fursa za ajira na kuwezesha uhamishaji wa teknolojia.[14] Muswada unahitaji angalau asilimia 80 ya bidhaa zinazozalishwa au kutengenezwa kwenye kanda maalum za kiuchumi lazima ziwe za kuuzwa nje. Mzunguko wa fedha kwa mwaka kwa kampuni hizo unatakiwa usiwe chini ya DOLA ZA KIMAREKANI dola za kimarekani 500,000[15] kwa wawekezaji wa nje na DOLA ZA KIMAREKANI 100,000 kwa wawekezaji wa ndani.

Mwaka 2006, serikali ilianzisha kanda maalum za kiuchumi (SEZs), ambazo zinajumuisha EPZs, Bandari huru, Kanda Huru za Biashara, Maeneo Tengwa ya Viwanda, Maeneo Tengwa ya Sayansi na Teknolojia, Kanda Huru za Kilimo na Kanda za Maendeleo ya Utalii. Wawekezaji hufaulu kuingia katika mpango wa kanda maalum za kiuchumi (SEZ) ikiwa wanaonesha kuwa uwekezaji wao ni mpya, wanafikia kiwango cha chini cha uuzaji wa nje cha DOLA ZA KIMAREKANI milioni 5 kwa wawekezaji wa nje na DOLA ZA KIMAREKANI milioni 1 kwa wawekezaji wa ndani, wanao mpango bora wa kulinda mazingira na wanatumia mbinu za kisasa za uzalishaji na utengenezaji wa bidhaa na mashine mpya na za kisasa.[16] Motisha za kodi katika EPZs na SEZs zinajumuisha:

- Msamaha wa kodi ya mapato ya makampuni kwa miaka 10 ya kwanza.

13 Tanzania Export Processing Zones Authority and the Export Processing Zones Act No. 11 of 2002; 'Corporate Tanzania: Business, Trade and Investment Guide 2010/2011', *www.corporate-tanzania.com*, pp.57, 99

14 Taarifa iliyopatikana kutokana na mahojiano binafsi na Afisa Uwekezaji wa Mamlaka ya Uwekezaji Tanzania. Tazama pia tovuti rasmi ya Mamlaka ya EPZs Tanzania. *http://www.epza.co.tz/About-EPZ-Program.html*

15 Kiwango cha ubadilishaji wa fedha kwa DOLA ZA KIMAREKANI kwenda shilingi ya Tanzania tarehe 3 Juni 2012 ilikuwa DOLA ZA KIMAREKANI 1 ni sawa na shilingi ya Tanzania 1600

16 Taarifa iliyopatikana kutokana na mahojiano binafsi na Afisa Mwezeshaji wa Mamlaka ya Uwekezaji Tanzania. Tazama pia tovuti rasmi ya Mamlaka ya EPZ Tanzania. *http://www.epza.co.tz/About-EPZ-Program.html*

- Msamaha katika kodi ya zuio kwenye upangaji, mgawo wa hisa, na faida kwa miaka 10 ya mwanzo.
- Msamaha wa ushuru wa uingizaji wa mali ghafi na bidhaa mtaji zinazoingizwa kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa katika kanda za uzalishaji wa bidhaa za kuuzwa nje (EPZs).
- Misamaha ya kodi la ongezeko la thamani (VAT) katika huduma za jamii na ushuru wa kutumia gati.
- Msamaha kwenye kodi zote na ushuru unaotozwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa miaka 10 ya mwanzo.
- Uhamishaji nje wa faida usio na kipimo.

Kati ya mambo yanayoleta wasiwasi katika muktadha huu wa misamaha ya kodi kwa "miaka 10 ya mwanzo" ni kwamba uwekezaji huu ulio rahisi-rahisi au usio na msingi imara mwanzoni, unaweza kuwa ni rahisi kwao kufunga shughuli zao baada ya kipindi cha msamaha wa kodi kuisha na kujiingiza tena kwenye maeneo mengine ya EPZs na SEZs ndani ya nchi kama uwekezaji mpya au hata kuondoka nchini na kwenda nchi nyingine . Hii ina maana kwamba hata baada ya miaka 10 ya msamaha wa kodi, hakuna hakikisho kwamba wawekezaji katika EPZs na SEZs watalipa kodi.

Motisha ya kodi kwa 'wawekezaji nyeti'

Utaratibu wa 'Mwekezaji Mwenye Hadhi ya Mwekezaji Nyeti' Tanzania, hutoa motisha mbalimbali ya kodi kwa makampuni yanayowekeza mitaji ya DOLA ZA KIMAREKANI zaidi ya milioni 20.

Kwa mujibu wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) 'Kwa mradi mkubwa unaozidi mtaji wa DOLA ZA KIMAREKANI milioni 20 na wenye kutoa manufaa maalum /makubwa kwa jamii au uchumi[17], wawekezaji wanaweza kuomba motisha maalum kutoka serikalini'[18]. Kwa hali hiyo baadhi ya makampuni hasa yale ya nje ya madini na makampuni ya kilimo cha biashara, yana mikataba binafsi ya kifedha na serikali, ambayo baadhi hutoa ridhaa maalum kwa makampuni binafsi lakini hayo hayajawahi kuwekwa wazi kwa umma. Huu ukosefu wa uwazi katika mikataba kama hiyo ni kati ya masuala nyeti katika muktadha wa utawala bora na usimamizi thabiti wa fedha za umma

17 Tuna maoni kwamba 'manufaa maalum kwa jamii au uchumi' yafafanuliwe zaidi ili kuondokana na hali inayojitokeza sasa ya tafsiri ya kudhania badala ya uhakika

18 'Investment incentives', *http://www.tic.co.tz/*

kwa ujumla na kwa namna ya pekee katika utozaji wa kodi kwa ajili ya kugharamia matumizi ya umma.

Motisha za Kodi kwa makampuni ya uchimbaji madini

Makampuni ya uchimbaji madini hupewa motisha na misamaha mbalimbali ya kodi. Haya yanajumuisha Mikataba ya uendelezaji wa Uchimbaji Madini ambayo Serikali imesaini nao. Ingawa sheria mpya ya uchimbaji madini iliyoanza kutumika mwaka 2010 - iliondoa sheria ya uchimbaji madini ya mwaka 1998 - Mikataba ya madini iliyowekewa sahihi kabla ya mwaka 2010 bado imebakia kuheshimiwa. Masharti yao mara nyingi hutofautiana, lakini mengi inaaminika (hayakuwekwa wazi kwa umma)[19] kuwa yana vipengele vya 'utulivu kifedha' (yaani vinavyozuia serikali isiongeze kodi)[20]. Hii inamaanisha kuwa wigo wa motisha za kodi zilizotolewa katika makubaliano binafsi zinauwezekano wa kuendelea kutumika hata chini ya sheria mpya. Misamaha ya kodi inayonufaisha makampuni ya uchimbaji madini inajumuisha;

- Asilimia sifuri katika ushuru wa mafuta (ukilinganisha na kiwango cha sasa cha ushuru wa shilingi za Tanzania 200 kwa lita moja) na katika vifaa vya uchimbaji madini vinavyoagizwa kutoka nje kuanzia wakati wa utafutaji wa madini hadi mwishoni mwa mwaka wa kwanza wa uzalishaji / uchimbaji; baada ya hapo wanalipa asilimia 5.
- Msamaha katika kodi itokanayo na ununuzi wa mali (tofauti na makampuni mengine hapa Tanzania)
- Unafuu malum katika kodi ya ongezeko la thamani, (VAT) kwenye

19 Haya ni baadhi ya maeneo ambapo uwazi unahitajika katika usimamizi wa fedha za umma

20 Mwezi Juni 2011, kwa mfano, taarifa ilitolewa kuwa serikali ilikuwa inafikiria kutoza 'kodi ya faida kubwa' juu ya mapato makubwa bila kutegemewa kutokana na uchimbaji madini. Lakini AngloGold Ashanti, iliyokuwa inachimba madini katika machimbo makubwa zaidi nchini ilisema kwamba uanzishaji wa kodi kama hiyo hautaleta tofauti yoyote katika ulipaji wake wa kodi kwani mkataba wake na serikali wa uchimbaji madini una kipengere cha 'utulivu kifedha' kinachokataza, serikali kuongeza kodi za kampuni. 'Documents confirm Tanzania is looking at mining "super profit tax"', Reuters, 8 June 2011; 'AngloGold says any Tanzanian "super profits" tax will not apply', Reuters, 8 June 2011

vifaa na mali inayoingizwa kutoka nje na ya humu ndani pamoja na huduma zitolewazo kwenye makampuni ya uchimbaji madini na wakandarasi wao wadogo wadogo.

- Uwezo wa kupunguza gharama za kodi ya mapato kwa kuingiza gharama ya vifaa/ bidhaa mtaji (mfano mashine mbalimbali na bidhaa nyinginezo zilizonunuliwa kwa shughuli za uchimbaji wa madini). Makampuni yasiyo ya madini yanastahili kupata asilimia 100 ya marupurupu ya uchakavu kwa miaka 5 tu ya kwanza ya shughuli.
- Punguzo la ushuru wa stempu kwa asilimia 0.3. Hii imeingizwa katika mikataba kadhaa iliyosainiwa kati ya serikali na makampuni ya uchimbaji madini, ingawaje kiwango cha ushuru wa stempu imewekwa kisheria kuwa ni asilimia 4.[21]
- Kiwango cha juu cha malipo ya kodi za serikali za mitaa cha hadi DOLA ZA KIMAREKANI 200,000 kwa mwaka, ambacho ni chini kwa kiasi cha asilimia 0.3 ya mzunguko wa kawaida kisheria.[22]
-

Motisha ya kodi kwa wawekezaji wa kilimo[23]

Wawekezaji katika Kilimo hupewa motisha zifuatazo:

- Ushuru-sifuri (hakuna) wa uingizaji bidhaa mtaji na pembejeo zote za shamba
- Kulegezwa kwa ushuru wa uingizaji wa mali ghafi zitakazotumika katika uzalishaji wa bidhaa kwa mauzo ya nje
- Kuahirisha kodi ya ongezeko la thamani kwa bidhaa mtaji ya mradi
- Kiwango-sifuri (hakuna) cha kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa bidhaa za kilimo za kuuza nje na kwa pembejeo za kilimo zinazozalishwa humu ndani

21 Tazama ' Mark Curtis and Tundu Lissu, *A Golden Opportunity: How Tanzania is Failing to Benefit from Gold Mining, October 2008',* kwa mjadala kuhusu motisha ya kifedha inayotolewa kwa makampuni ya uchimbaji madini na kwa vyanzo vyote katika sehemu zinazofuata.

22 Tazama 'Mark Curtis and Tundu Lissu, *A Golden Opportunity: How Tanzania is Failing to Benefit from Gold Mining, October 2008* kwa mjadala kuhusu motisha ya kifedha inayotolewa kwa makampuni ya uchimbaji madini na kwa vyanzo vyote katika sehemu zinazofuata.

23 Tazama 'Corporate Tanzania: Business, Trade and Investment Guide 2010/2011', *www.corporate-tanzania.com*, p.72'

Misamaha zaidi ya kodi hutolewa chini ya mpango wa '*Kilimo Kwanza'* [24] wenye lengo la kufanya kilimo kiwe cha kibiashara na chenye kutumia teknolojia ya kisasa.[25]

- Kodi ya ongezeko la thamani inasamehewa kwa idadi kadhaa ya vitu kama vile mafuta yanayohitajika kwa usafirishaji wa mazao ya kilimo k.m. miwa, katani na chai kutoka shambani hadi kiwanda cha usindikaji, chakula cha mifugo na mashine za kilimo kama vile mashine za kuvuna nafaka.
- Ushuru wa kuingiza matrekta umesamehewa.

Misamaha mingine ya kodi

Makampuni yaliyoorodheshwa hivi karibuni katika soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) yenye angalau asilimia 30 ya hisa zao zilizouzwa kwa umma hulipa asilimia 25 tu kodi ya **mapato ya makampuni** (ukilinganisha na kiwango cha asilimia 30 kisheria) kwa miaka mitatu ya mwanzo.[26]

Hisa za makampuni yaliyoorodheshwa kwenye soko la mtaji la Dar es Salaam husamehewa kulipia **kodi ya faida ya kimtaji** ambayo kiwango chake cha kawaida ni asilimia 30).[27]

Kuna idadi kadhaa ya vitu vilivyosamehewa kodi ya ongezeko la thamani zaidi ya vile vilivyotajwa hapo juu. Hivi vinajumuisha, lakini

---

24 Iliyoanzishwa na sekta binafsi mwaka 2009.

25 Katika bajeti ya 2011/12 , Waziri wa Kilimo alisema kwamba Kilimo Kwanza inategemewa kuongeza ajira, hususan kwa vijana vijijini, na Benki ya Dunia ina mpango wa kugharimia mpango huu kwa kutoa DOLA ZA KIMAREKANI milioni 60, inayolingana na Tshs bilioni 92.8 billion; http://www.mof.go.tz. Misamaha ina mwelekeo wa kuwanufaisha wakulima wa kibiashara kubwa na kuwaacha Watanzania walio wengi ambao ni wakulima wadogo wa kilimo cha kujikimu. Misamaha ya VAT katika mafuta , kwa mfano, huwanufaisha wakulima waliojipanga katika vikundi na siyo wakulima wadogo wadogo binafsi wakati misamaha ya ushuru wa uingizaji wa matrekta haina maana kwa wakulima wadogo ambao hawana uwezo wa kununua vifaa kama hivyo ambavyo hata hivyo havifai kwa kilimo cha mashamba madogo. Policy Forum, 'Do Kilimo Kwanza Exemptions Benefit Poor Farmers?', Policy Brief 3:10, 2010

26 *TRA, Taxes and Duties at a Glance 2010/2011*, p.1

27 *TRA, Taxes and Duties at a Glance 2010/2011*, p.2; PKF, Tanzanian Tax Guide 2010, p.1

siyo hivi tu: bima, elimu, huduma ya kifedha na huduma za kitalii. Bidhaa zinazotolewa chini ya msaada wa kitekenolojia au miradi inayogharimiwa na wahisani au mashirika ya kujitolea zimesamehewa kodi ya ongezeko la thamani.[28]

Motisha za kodi kwa wanaowekeza Zanzibar [29]

Zanzibar imeunda Kanda Huru za Kiuchumi (FEZs) na Bandari Huru, vile vile inawapa wawekezaji motisha mbalimbali, zilizo muhimu ni pamoja na:

- Msamaha wa kodi ya mapato ya makampuni (ndani ya EPZ: asilimia 100 kwa miaka 10 ya mwanzo, kisha asilimia 75 kwa miaka 10 inayofuatia; Katika Bandari Huru: asilimia 100 kwa miaka 20 ya mwanzo)
- Msamaha kwenye ushuru wa uingizaji bidhaa kama vile mashine, vifaa na mali ghafi za ujenzi
- Msamaha wa kodi kwa bidhaa zinazouzwa nje
- Msamaha wa kodi kwenye mgawo wa faida kwa miaka 10 ya mwanzo (kwenye kanda huru za kiuchumi - yaani EPZ pekee)
- Msamaha wa kodi zote za ndani kwa bidhaa zinazozalishwa ndani ya kanda

28 TRA, Taxes and Duties at a Glance 2010/2011, p.6

29 'Corporate Tanzania: Business, Trade and Investment Guide 2010/2011', p.116, *www.corporate-tanzania.com*

7. Wanaonufaika na wanaoathirika kutokana na Motisha za Kodi

Ukosefu wa uwazi katika motisha za kodi, kwa muda mrefu umezuia umma usiweze kuzichambua kwa kina. Hata hivyo uchambuzi unaonesha kuwa washindi wakuu (wanaonufaika) wa motisha za kodi na misamaha katika Tanzania ni kundi dogo la wawekezaji wa nje. Wanaoathirika– kutokana na upotevu mkubwa wa mapato – ni umma kwa ujumla na nchi yote. Motisha za kodi zinazofurahiwa na wanaonufaika humaanisha faida zaidi na migawo mizuri zaidi kwa wenye hisa. Fedha zilizopotea kupitia motisha hizi humaanisha fedha ambazo hazitapatikana tena kugharamia matumizi ya umma katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mengine: Elimu ya umma, afya, miundo mbinu, maji na usalama.

Kuna makisio tofauti tofauti yanayoonesha upotevu wa mapato uliosababishwa na motisha na misamaha ya kodi Tanzania:

- Taarifa ya Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) inaonesha kuwa misamaha na motisha imefikia kiwango cha asilimia 6 ya Zao Ghafi la Ndani (GDP) au shilingi za Tanzania trilioni 1.8 (DOLA ZA KIMAREKANI bilioni 1.23) mwaka 2008.[30]
- Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki – ikifuatilia misamaha ya ushuru wa uingizaji tu – inakisia kuwa upotevu wa mapato kutokana na misamaha ya kodi ilifikia DOLA ZA KIMAREKANI milioni 435.9 (TShs bilioni 955) mwaka 2008 na wastani wa DOLA ZA KIMAREKANI milioni 370 (TShs bilioni 811) katika miaka mitatu 2006-08.[31]
- Uchambuzi uliofanywa na Asasi isiyo ya kiserikali (AZAKI) la Uwazi, kwa kutumia takwimu toka Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA) inaonesha kuwa upotevu kutokana na motisha na misamaha umefikia Shilingi za Tanzania bilioni 752 kwa mwaka 2008/09 na Shilingi za Tanzania bilioni 695 kwa mwaka 2009/10.[32]

30 African Development Bank, Domestic Resource Mobilisation for Poverty Reduction in East Africa: Tanzania Case Study, November 2010, p.20

31 The EAC Trade Report, 2009, *http://www.eac.int/statistics/index.php?option*

32 Uwazi, 'Tanzania's Tax Exemptions: Are they too high and making us too dependent on Foreign Aid?', Policy Brief, TZ.12/2010E, p.3

Kwa mujibu wa uchambuzi wa Asasi ya Uwazi, wafaidikaji wakubwa wa hizi motisha na misamaha ni wale wenye vyeti vya uwekezaji kutoka Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Ukuzaji wa Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) ambazo kwa pamoja zimefikia asilimia 45 ya misamaha na motisha kwa miaka 2008/09 – 2009/10; haya ni makampuni ya kimataifa-mtandao.[33] Makampuni ya kuchimba madini nayo yalikuwa asilimia 7.5 ya waliofaidika. Kwa hiyo kwa pamoja makampuni haya yamefikia karibu asilimia 52 ya jumla ya motisha na misamaha ya kodi iliyotolewa. Hii inafikia shilingi za Tanzania bilioni 381 kwa miaka ya fedha 2008/09 – 2009/10

Aina ya misamaha Iliyotolewa 2008/09 – 2009/10 kwa aina



Chanzo: Uwazi, 'Tanzania's Tax Exemptions: Are they too high and making us too dependent on Foreign Aid?', *Policy Brief*, TZ.12/2010, p.5

33 Uwazi, 'Tanzania's Tax Exemptions: Are they too high and making us too dependent on foreign aid?', Policy Brief, TZ.12/2010E, pp.1, 5

Masuala kuhusu misamaha ya kodi katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ya mwaka 2010/11.[34]

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa mwaka 2010/11 imeainisha masuala kadhaa kuhusiana na kodi kwa ujumla na misamaha ya kodi kwa msisitizo. Masuala makuu yanajumuisha yafuatayo:

i. Mahesabu ya mapato ya kodi kwa Tanzania Bara yalifungwa na makusanyo halisi ya Sh. 5,550,205,244,378 dhidi ya makisio yaliyopitishwa ya shilingi 5,849,093,700,000; hivyo kusababisha upungufu wa makusanyo ya shilingi 298,888,455,622.
ii. Taarifa ya Mapato ya TRA ilionesha kuwa misamaha ya kodi imefikia Sh.1,016,320,300,000 sawasawa na asilimia 18 ya jumla ya makusanyo yote. Ilionekana kwamba kama kiasi hicho kisingeenda katika misamaha ya kodi, jumla ya makusanyo ingeongezeka na kufikia kiasi cha sh. 6,566,525,544,378; hivyo ingesababisha makusanyo ya ziada kufikia Sh.717,431,844,378.

Kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu (CAG), taarifa ya mapato ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilionesha kuwa misamaha ya kodi ilifikia Sh.1,016,320,300,000. Misamaha hiyo ilitolewa kwa taasisi kama zinavyooneshwa kwenye jedwali 2:

34 Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu Kuhusu Ukaguzi wa Taarifa ya Fedha ya Serikali Kuu kwa Mwaka uliomalizika 30 Juni, 2011

Jedwali 2 :Muhtasari wa misamaha ya kodi iliyotolewa kwa taasisi kwa mwaka wa fedha 2010/11

Taasisi	Idara ya Forodha na Ushuru (Shs)	Idara ya Mapato ya Ndani (Shs)	Jumla (Shs) 2010/2011	Jumla (Shs) 2009/2010
Taasisi za Kiserikali	35,867,200,000	-	35,867,200	52,743,800,000
Mashirika ya Umma	8,131,200,000	-	8,131,200,000	8,758,700,000
Taasisi za dini	1,569,300,000	-	1,569,300,000	281,200,000
AZAKI	25,462,600,000	-	25,462,600,000	22,147,100,000
Miradi inayofadhiliwa na wahisani	115,758,100,000	-	115,758,100,000	72,458,100,000
Makampuni binafsi na watu binafsi	182,706,100,000	-	182,706,100,000	36,174,600,000
Sekta ya Madini	109,885,900,000	-	109,885,900,000	48,738,600,000
Misamaha ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania	239,667,300,000	-	239,667,300,000	268,002,300,000
Misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Chini ya Maduka yasiyotozwa Ushuru		17,427,400,000	17,427,400,000	2,691,600,000
Jumla	**719,047,700,000**	**297,272,600,000**	**1,016,320,300,000**	**680,667,900,000**

Chanzo:Ripoti ya mkaguzi na mdhibiti mkuu 2010/11, uk. 50 – 51.

Takwimu kutoka kwenye taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu (CAG) inaonesha ongezeko la misamaha kwa Sh. 335,652,400,000 au 49% kutoka Sh 680,667,900,000 kwa taarifa ya mwaka wa fedha 2009/2010 hadi Sh. 1,016,320,300,000 kwa taarifa ya mwaka 2010/2011. Msamaha wa Sh. 1,016,320,300,000 ni 18% ya makusanyo halisi. Kwa mujibu wa CAG, kama fedha hizi zingekusanywa kama kodi, taarifa iliyotolewa ya makusanyo pungufu ya fedha ya Sh.298,888,455,622 kwa Tanzania Bara ingeweza kufutwa. Hii ingeacha ziada ya makusanyo ya shilingi 717,431,844,378.

Masuala ya misamaha ya kodi katika bajeti ya mwaka 2010/11

Kama ilivyokuwa kwa miaka mingine mingi, serikali ilitoa motisha kadhaa katika mwaka 2010/11. Baadhi ya hizi zimeorodheshwa kama ifuatavyo:

i) Msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye vipuri vya zana za kilimo ikiwa ni pamoja na vipuzia nafaka, vikaushaji na mashine ya usagishaji, mashine za kupandia mbegu na pawatila (trekta ndogo za kusukuma kwa mkono)

ii) Msamaha wa VAT kwenye chakula cha mifugo (NASCOR Pellet Feed)

iii) Msamaha wa VAT kwenye kitani ya nailoni ya kuvulia samaki

iv) Msamaha wa VAT kwenye pampu za kupulizia, harro, mitambo ya kupitishia nafaka

v) Ufidiaji wa kodi kwenye manunuzi ya rejareja yanayofanywa na wageni kwa manunuzi yanayofikia sh. 400,000

vi) Msamaha wa kodi kwenye posho zinazolipwa kwa watumishi wa serikali na wale wanaofanya kwenye taasisi zinazopewa ruzuku na serikali

vii) Kupunguza tozo kwenye mafuta mazito ya kuendesha mitambo kutoka Shilingi za Tanzania 80 kwa lita hadi Shilingi za Tanzania40 kwa lita kwa ajili ya kupunguza gharama za uzalishaji

viii) Kutoza ushuru wa 50% badala ya 120% kwenye bidhaa aina ya 'Polymers of ethylene' na bidhaa nyingine zenye HS. Code 3923.2900"

ix) Msamaha wa kodi kwenye ushuru wa petroli inayotumika katika utafiti wa utafutaji madini

Kwa ujumla misamaha katika Tanzania Bara inaonesha mwelekeo wa kuongezeka kama inavyooneshwa kwa kiasi fulani katika jedwali (lifuatalo) hapa chini:

Jedwali 3: Misamaha kwa miaka 2011/12 na 2009/10

Maelezo	**2011/2012**	**2009/2010**
Makusanyo halisi	5,550,205,244,378	4,637,686,999,618
Misamaha	1,016,320,300,000	680,667,900,000
Kiwango cha misamaha ikilinganishwa na makusanyo halisi	18%	15%
Pungufu katika makusanyo	298,888,455,622	391,235,100,382
Ziada kama misamaha isingetolewa	717,431,844,378	289,432,799,618

Kiwango cha misamaha ya kodi Tanzania kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa mwaka 2010/11 au ulioishia Juni 2011, iko juu ikilinganishwa na nchi zingine kama vile Kenya na Uganda.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ana wazo sahihi kwamba Tanzania, maskini kama ilivyo, haina uwezo wa kupoteza mapato yake yanayohitajika sana kwa kuruhusu misamaha mikubwa ya kodi. Mara nyingi, kwa mujibu wa taarifa ya CAG, misamaha imetolewa kwa watu wenye uwezo na makampuni makubwa ya kimataifa yenye rasilimali zote. Kwa hiyo, siyo busara kutegema mno misaada ya wahisani [35] wakati huo huo nchi inatoa misamaha ya kodi ambayo ingekusanywa ili kugharimia matumizi ya umma kwenye bidhaa na huduma kwa bajeti zote, ya miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida. Ingawaje misamaha hiyo inatawaliwa na sheria ya kodi, kuna hitaji la kuhakikisha kuwa misamaha hiyo inatolewa kwa manufaa mapana ya umma.

Kwa mujibu wa gazeti la Citizen la Jumatano tarehe 4 Aprili 2012, bajeti

35 Bajeti ya mwaka 2011/12 ilikuwa tegemezi kwa wahisani kwa kiwango cha 28.%.

iliyopangwa kwa mwaka 2012/13 ni shilingi za Tanzania trilioni 13.5[36]. Kwa hiyo, mwaka 2011 jumla ya misamaha ilifikia shilingi trilioni 1.02 ambayo ni 7.6 % ya jumla ya bajeti iliyopangwa kwa mwaka 2012/13. Ilikadiriwa katika bajeti iliyopangwa kwa mwaka 2012/13 kwamba jumla ya shilingi za Tanzania bilioni 7,466 zitatoka katika vyanzo vya kodi na vingine visivyo vya kodi. Hii ni pungufu ya Shilingi za Tanzania trilioni 1.02 zilizosamehewa mwaka 2011. Mpango wa bajeti ya mwaka 2012/13 unaonesha kuwa kiasi cha Shilingi za Tanzania bilioni 3,397 zinategemewa kutoka kwa wahisani kama ruzuku na mikopo. Hizi Shilingi za Tanzania Trilioni 1.02 ambazo zilisamehewa mwaka 2011 ni nyingi zaidi ya fedha zinazotegemewa kutoka kwa wahisani kwa bajeti ya mwaka 2012/13. Kwa mujibu wa gazeti iliyotajwa hapo juu, mpango wa serikali ilikuwa kukopa kiasi cha Shilingi za Tanzania bilioni 2,292 katika bajeti ya mwaka 2012/13. Hii vile vile ni ndogo ukilinganisha na Shilingi za Tanzania trilioni 1.02 iliyosamehewa mwaka 2011. Mpango kwa bajeti ya mwaka 2012/13 ni kutumia Tsh trilioni 9.3 kwa matumizi ya kawaida. Kiasi cha kodi iliyosamehewa cha Shilingi za Tanzania trilioni 1.02 ni kama 11% ya bajeti ya kawaida. Mpango wa bajeti kwa mwaka 2012/13 ni kutumia Tsh trilioni 4.1 kwa matumizi ya maendeleo. Kiasi cha kodi iliyosamehewa kwa mwaka 2011 ni 24.9 % ya bajeti iliyopangwa kwa matumizi ya maendeleo kwa mwaka 2012/13.[37]

Tukizingatia makisio mbalimbali, hitimisho letu ni kwamba upotevu wa fedha za mapato kutokana na *misamaha yote na motisha zote* za kodi inaweza kuwa juu kufikia kiasi cha shilingi trilioni 1.8 (DOLA ZA KIMAREKANI bilioni 1.23) kwa mwaka 2008 (Kwa mujibu wa makisio ya Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), na kwamba *kiwango cha chini* cha upotevu wa mapato kutokana na *motisha za kodi* zinazotolewa kwa makampuni peke yake ni kama shilingi za Tanzania bilioni 381 b (DOLA

36 Wakati taarifa hii ilipokamilika, hotuba ya Waziri wa Fedha, Mipango na Uchumi kuhusu bajeti ya mwaka 2012/13 ilikuwa haijatolewa. Kwa hiyo takwimu zilizotolewa Aprili 2012 zinaweza kuwa tofauti kidogo na zile za kwenye hotuba rasmi ya bajeti iliyotolewa katikati ya mwezi Juni.

37 Masuala ya misamaha ya kodi katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu zimeandikwa katika vyombo vya habari. Sehemu moja ambapo taarifa hizi zipo ni katika mtandao: *http://mobile.theeastafrican.co.ke/Business/Tanzania+loses+460m+US+dollars+surplus+to+tax+exemptions+/-/433844/1390978/-/format/xhtml/-/3732n/-/index.html*

ZA KIMAREKANI milioni 174) kwa mwaka (kwa miaka ya 2008/09 – 2009/10). Kwa mwaka 2011/12, takwimu kwa misamaha mahususi ni kama zilivyooneshwa katika jedwali namba moja.

Makadirio ya Upotevu wa Mapato Kutokana na Misamaha na Motisha za Kodi

Hapa chini kuna makadirio ya upotevu wa mapato kutokana na misamaha na motisha za kodi kama zilivyotolewa toka kwenye vyanzo mbalimbali. Kuna sababu mbalimbali za tofauti za takwimu. Sababu hizi zinajumuisha (lakini si sababu pekee) zifuatazo: tofauti katika vyanzo vya awali vya taarifa, tofauti katika mbinu za kukokotoa mahesabu na makadirio ya makosa. Ni nje ya malengo ya utafiti huu kuainisha sababu halisi za tofauti zilizojitokeza katika takwimu zilizotolewa.

Kisanduku 2: Makadirio mbalimbali ya upotevu wa mapato kutokana na misamaha na motisha za kodi

Serikali

Hotuba za bajeti ya serikali zinakadiria kuwa *misamaha ya kodi* ilifikia kiasi cha 2.5% ya Zao Ghafi la Ndani kwa mwaka 2010/11 asilimia 3.5 kwa mwaka 2007/08 (inayofuata ikiwa ni asilimia 30 ya jumla ya mapato yote ya kodi.).[38] Kwa mwaka 2010/11, mahesabu yetu ni kwamba hii itakuwa kama Shilingi za Tanzania bilioni 866 (DOLA ZA KIMAREKANI milioni 395).[39] Katika miezi sita ya mwanzo ya mwaka 2010, serikali ilikadiria kuwa *misamaha ya kodi* ilifikia kama theluthi moja ya jumla ya kodi zilizokusanywa, au Shilingi za Tanzania bilioni 833 (DOLA ZA KIMAREKANI milioni 480).[40] Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikadiria kuwa upotevu wa mapato unaotokana na *misamaha ya kodi* ulikuwa Shilingi za Tanzania bilioni 587 (DOLA ZA KIMAREKANI milioni 403) kati ya Julai 2008 hadi Aprili 2009.[41]

38 Finance Minister, Budget Speech 2011/12, p.25; Budget Speech 2009/2010, para. 78, *http://www.mof.go.tz*

39 Based on nominal GDP projection of TShs 34,656 billion. IMF, Staff Report for the 2011 Article IV Consultation and Second Review under the Policy Support Instrument, 21 April 2011, p.24

40 IMF, Staff Report for the 2011 Article IV Consultation and Second Review under the Policy Support Instrument, 21 April 2011, p.36

41 African Development Bank, Domestic Resource Mobilisation for Poverty Reduction in East Africa: Tanzania Case Study, November 2010, p.20

Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF)

IMF inakadiria kwamba *misamaha ya kodi* inagharimu serikali 3.5% ya Zao Ghafi la Ndani (GDP) kwa mwaka.[42] Mahesabu yetu ni kwamba hii ni sawa na Shilingi za Tanzania trilioni 1.06 (DOLA ZA KIMAREKANI milioni 611) kwa mwaka.[43]

Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB)

Taarifa ya AfDB inaonesha kuwa misamaha na motisha zinafikia hadi 6% ya Zao Ghafi la Ndani (GDP) au, Shilingi za Tanzania trilioni 1.8 (DOLA ZA KIMAREKANI bilioni 1.23) mwaka 2008.[44]

Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki

Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) – ikielezea juu ya *misamaha ya ushuru wa uaigizaji bidhaa nje peke yake* - inakadiria kuwa mwaka 2008, Upotevu wa mapato ya Tanzania kutokana na misamaha ya kodi ilifikia kiasi cha DOLA ZA KIMAREKANI milioni 435.9, na wastani wa DOLA ZA KIMAREKANI 370 milioni katika miaka mitatu 2006-08.[45]

Misamaha ya ushuru wa uingizaji bidhaa iliyotolewa na Tanzania 2005-2008 (Milioni kwa Dola ya Marekani)

	2005	2006	2007	2008
Thamani ya misamaha	901.6	1225.9	1496.2	1826.1
Mapato yaliyoachiliwa	204.2	405.4	268.3	435.9
Jumla ya kodi za Biashara	730.5	822.1	1104.7	1440.9
Asilimia zilizoachiliwa	21.8	33.0	19.5	23.2

Chanzo: EAC Secretariat, *EAC Trade Report 2008*, 2010, p.51

42 IMF, Staff Report for the 2011 Article IV Consultation and Second Review under the Policy Support Instrument, 21 April 2011, p.14

43 Based on figures in IMF, Staff Report for the 2011 Article IV Consultation and Second Review under the Policy Support Instrument, 21 April 2011, p.24. Nominal GDP of TShs of 30,321 billion.

44 African Development Bank, Domestic Resource Mobilisation for Poverty Reduction in East Africa: Tanzania Case Study, November 2010, p.20

45 The EAC Trade Report, 2009, *http://www.eac.int/statistics/index.hp?option*

Uwazi

Azaki ya Uwazi, inakadiria, kwa kutumia vyanzo vya TRA, kwamba *misamaha ya kodi* ilikuwa wastani wa 3.9% ya Pato la Taifa kati ya 2005/06 – 2007/08 na ilikuwa 2.8% mwaka 2008/09 na 2.3% mwaka 2009/10. Katika mwaka uliofuatia, misamaha ilifikia kiasi cha Shilingi za Tanzania bilioni 695 yaani (DOLA ZA KIMAREKANI milioni 417 million).[46] Kiasi cha misamaha imeongezeka sana kipindi cha 2006-10: Katika miaka hiyo mitano, upotevu wa mapato kutokana na misamaha ilifikia kiwango kikubwa cha Shilingi za Tanzania Trilioni 3.87 (DOLA ZA KIMAREKANI bilioni 2.3

Misamaha ya Kodi Tanzania, 2000-2010



	2000	2001	2001	2003	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010
Misamaha	218	201	250	231	316	459	772	840	814	752	695

Chanzo:Uwazi, 'Tanzania's Tax Exemptions: Are they too high and making us too dependent on Foreign Aid?', *Policy Brief*, TZ.12/2010E, p.3

Misamaha ya kodi kwa uwiano wa Pato la Taifa



Chanzo:Uwazi, 'Tanzania's Tax Exemptions: Are they too high and making us too dependent

46 Uwazi, 'Tanzania's Tax Exemptions: Are they too high and making us too dependent on foreign aid?', Policy Brief, TZ.12/2010E, pp.2-3

Upotevu wa Mapato katika Sekta ya Madini

Ikizingatiwa kuwa Tanzania ni mmoja ya nchi za Afrika zinazozalisha madini kwa wingi, matarajio yalikuwa sekta ya madini ingetoa mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi. Hata hivyo matarajio hayo hayajafikiwa. Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) unataarifu kuwa mauzo ya nje ya dhahabu yameongezeka kutoka kiasi cha DOLA ZA KIMAREKANI milioni 500 hadi DOLA ZA KIMAREKANI billioni 1.5 katika miaka mitano iliyopita kutokana na upandaji wa bei ya dhahabu, lakini mapato ya serikali yamebakia kiasi cha kama DOLA ZA KIMAREKANI milioni 100 kwa mwaka. Hii kwa sehemu kubwa imesababishwa na misamaha ya kodi kwa makampuni makubwa iliyotolewa kwa makampuni ya madini. Ukweli ni kwamba, 'hakuna hata kampuni mmoja kati ya makampuni ya dhahabu yaliyopo imelipa kodi husika ya mapato hadi leo hii, kwa mujibu wa IMF.[47] Zaidi ya hayo, mapato ya madini hayatapanda sana tena siku za karibuni: kwa mujibu wa IMF, 'Sekta ya madini inayokua imekuwa hadi sasa na mabadiliko kidogo sana katika faida kifedha na hali haitegemewi kubadilika katika miaka inayokuja, kwa kiasi fulani hali hii inasababishwa na malimbikizo ya misamaha ya kodi.'[48] Kama ilivyooneshwa, ingawa sheria mpya ya madini ilipitishwa mwaka 2010, migodi ya dhahabu iliyopo inaendelea kusimamiwa na mikataba yao iliyokuwepo tangu awali.

Mapato yaliyopotea kutokana na motisha za kodi zilizotolewa kwa makampuni ya madini yana umuhimu, ingawaje takwimu za jumla hazijawahi kupigiwa mahesabu.

- Tume ya Bomani ilikisia kuwa serikali imepoteza Shilingi za Tanzania bilioni 39.8 mwaka 2006/7 na Shilingi za Tanzania bilioni 59 mwaka 2007/8 kutokana na **msamaha wa ushuru kwenye mafuta** uliotolewa kwa makampuni makubwa sita ya madini.[49] Hivi karibuni, 2011, makampuni ya madini yalikuwa yakidai serikali fidia ya kiasi cha DOLA ZA KIMAREKANI milioni 274 inayohusiana na msamaha wa ushuru mafuta kwa kipindi cha tangu 2002.[50]

47 IMF, *Staff Report for the 2011 Article IV Consultation and Second Review under the Policy Support Instrument*, 21 April 2011, p.17

48 IMF, *Staff Report for the 2011 Article IV Consultation and Second Review under the Policy Support Instrument*, 21 April 2011, p.14

49 Policy Forum, 'How Much Revenue Are We Losing?', *Policy Brief*, March 2009

50 David Malingha Doya, 'Tanzania May Abolish Tax Refund for Miners to Boost Revenue', 25 October 2011, www.bloomberg.com

- Makampuni ya madini yana umiliki haki usioingiliwa wa uendeshaji wa shughuli zao na madini yanayopatikana na uwezo wa kuyaondoa wanavyotaka, ikiwa ni pamoja na hata kuhamisha hizo haki kwa makampuni mengine bila kulipia kodi ya faida ya kimtaji. Hii ina maanisha kuwa ununuzi na uuzaji wa haki za uchimbaji wa madini unaweza kuwa na faida kubwa.[51]

- Uwezo wa makampuni ya madini **kufidia dhidi ya mapato wanayopashwa kulipia kodi,** gharama kamili katika matumizi kama vile ya mitambo na mashine imepelekea upotevu wa kodi. Kutokana na hali hii mwaka 2008 serikali ilianzisha Kodi Mbadala ya kima cha chini cha 0.3% ya mzunguko wa fedha wa kampuni inayolipwa pale ambapo makampuni yametamka hasara ya kodi kwa miaka mitatu mfululizo, ingawa kuna uwezakano mkubwa kuwa mapato yanayopatikana kutokana na kodi hii ni madogo sana ukilinganisha na upotevu unaotokana kwenye mtaji wa uwekezaji na misamaha ya kodi.

Kisanduku 3: Mifano Iliyochaguliwa ya Motisha ya Kodi kwa Makampuni ya Madini

- Uwezo wa makampuni ya madini **kufidia dhidi ya mapato wanayopaswa kulipia kodi,** gharama kamili katika matumizi kama vile ya mitambo na mashine imepelekea katika matamko yasiyokoma ya upotevu wa kodi, kwa hiyo kutokulipa kodi ya mapato ya kampuni. Kutokana na hali hii mwaka 2008 serikali ilianzisha Kima cha Chini cha Kodi Mbadala ya 0.3% ya uzalishaji inayolipwa pale ambapo makampuni yametamka hasara ya kodi kwa miaka mitatu mfululizo, ingawa kuna uwezakano mkubwa kuwa mapato yanayopatikana kutokana na kodi hii ni madogo sana ukilinganisha na upotevu unaotokana na marupurupu ya mtaji.

51 Mwaka 2003, kwa mfano, Kampuni ya Australia, East African Gold Mines, ilipata DOLA ZA KIMAREKANI milioni 252 kwa kuuza mgodi mmoja wa dhahabu wa Tanzania kwa kampuni ya Canada, Placer Dome (ambayo baadaye ilinunuliwa na Barrick), kutoka uwekezaji wa awali wa DOLA ZA KIMAREKANI milioni 90. Serikali ya Tanzania wala wananchi hawajapokea cho chote kutokana na haya mahusiano ya kibiashara ya mamilioni ya dola. Tundu Lissu, '"Conducive environment" for whose development?: Globalisation, national economy and the politics of plunder in Tanzania's mining industry', unpublished paper, November 2006, pp.16-17

- Tume ya Bomani iliyoundwa na serikali ilikadiria kuwa nchi ilipoteza Shilingi za Tanzania bilioni 39.8 mwaka 2006/7 na TShs bilioni 59 mwaka 2007/8 **kwa ajili ya misamaha ya kodi ya mafuta** iliyotolewa kwa makampuni makubwa sita.[52] Hadi karibu na mwisho wa mwaka 2011, makampuni ya uchimbaji madini yalikuwa yanadai serikali fidia ya kiasi cha DOLA ZA KIMAREKANI milioni 274 kuhusu misamaha ya kodi yao ya mafuta kwa kipindi cha kuanzia 2002.[53]

Madai ya kifedha katika *sekta* ya madini

Mnamo mwaka 2010, Wakala na Mkaguzi wa Madini (TMAA) ilikagua makampuni ya madini 12[54] na kutoa hoja kadhaa za ukaguzi kuhusiana na madai ya kifedha ya makampuni hayo. Ilitoa taarifa kwamba makampuni ya madini hayo yalitamka kiwango cha juu sana kwenye kodi ya ya mtaji wa uwekezaji (capital allowance) na gharama za uendeshaji. Jedwali hapa chini linaonesha hoja za ukaguzi ambazo hazikupata maelezo ya kuridhisha.

52 In 2003, for example, the Australian company, East African Gold Mines, made US$252 million by selling one Tanzanian gold mine to the Canadian company Placer Dome (which was later bought by Barrick), from an original investment of US$90 million. Neither the government of Tanzania nor ordinary citizens receive anything from these multi-million dollar deals. Tundu Lissu, '"Conducive environment" for whose development?: Globalisation, national economy and the politics of plunder in Tanzania's mining industry', unpublished paper, November 2006, pp.16-17

53 Based on figures in Uwazi, 'Tanzania's Tax Exemptions: Are they too high and making us too dependent on foreign aid?', Policy Brief, TZ.12/2010E, p.2

54 Geita Gold Mine Ltd, Tanzanite One Mining Ltd, Bulyanhulu Gold Mine Ltd, Pangea Minerals Ltd, North Mara Gold Mine Ltd, Resolute Tanzania Ltd, Williamson Diamond Ltd, Tanzania Oxygen Ltd, El Hillal Minerals Ltd, Mbeya Cement Company Ltd, Tazaro Kongoro Quarry and one unspecified holder of a Dealers Licence

Jedwali 4: Hoja muhimu za ukaguzi zilizotolewa na TMAA kwa makampuni ya uchimbaji madini, 2010

Madai yasiyo sahihi ya madeni ya kinga dhidi ya hasara na upotevu wa kifedha	$183.6 milioni
Marupurupu mtaji yaliyodaiwa zaidi ya kiasi halisi	$179.3 milioni
Mtaji na gharama za uendeshaji zisizo na vithibitisho	$141.2 milioni
Vifaa / zana visivyoruhusiwa	$53.8 milioni na TShs 1.7 bilioni
Madai yasiyo sahihi na punguzo la mtaji la kabla ya wakati	$44.5 milioni
Mauzo ya madini yaliyo chini ya kiasi halisi	$12.4 milioni na TShs 3.0 bilioni
Malipo ya huduma ya kitaalamu ambapo zuio la kodi halikuzuiwa	$50.9 milioni na TShs 1.5 bilioni
Ada ya menejimenti ambapo zuio la kodi halikuzuiwa	$23.1 milioni
Malipo ya mishahara yaliyo juu zaidi ya malipo halisi	$9.9 milioni
Ulipaji wa chini wa ushuru wa maendeleo ya stadi	$1.7 milioni
Mrabaha (Malipo ya mwandishi ambayo hayajalipwa	$0.2 milioni na TShs 466 milioni
Kodi ya mapato (PAYE) zisizolipwa.	TShs 911 milioni
Kodi za mwaka za pango zisizolipwa kwa haki za madini zilizotolewa	0.5 milioni
Jumla	**$705.8 milioni**

Chanzo: TMAA, *Annual Report 2010*, p.3

Hoja za ukaguzi zisizopatiwa ufumbuzi

Wakati Wakala na Mkaguzi wa Madini Tanzania (TMAA) inaposhindwa kupatia ufumbuzi masuala na makampuni ya uchimbaji wa madini hoja hizo zinawasilishwa kwa TRA. Chini kuna hoja kuu za ukaguzi wa makampuni ya madini zisizopatiwa ufumbuzi zilizowasilishwa na TMAA kwa TRA mwaka 2010.

Jedwali 5: Hoja za ukaguzi ambazo hazijapatiwa ufumbuzi zilizotolewa na TMAA kwa TRA.

Madai yasiyo sahihi ya mtaji na gharama za uendeshaji kwa lengo la kodi	$119.2 milioni
Madai yasiyo sahihi ya kinga dhidi ya madeni na upotevu wa fedha	$75.3 milioni
Vitu visivyoruhusiwa vikidaiwa kama gharama zinazoruhusiwa	$53.3 milioni
Makato ya madai ya uchakavu yanayozidi kiwango halisi	$3.3 milioni
Jumla	**$251.1 milioni**

Chanzo: TMAA, *Annual Report 2010*, p.37

Kiasi cha DOLA ZA KIMAREKANI milioni 705 zinamaanisha (dhima) deni la kodi lililo kubwa zaidi. Ukaguzi wa madini wa mwaka 2003 ulidai kwamba deni la kweli la kodi inafikia kiasi cha kama robo ya takwimu iliyotolewa ya hasara iliyokuwa imekuzwa sana. Kwa hiyo kiasi cha DOLA ZA KIMAREKANI milioni 705 inamaanisha deni la kodi la DOLA ZA KIMAREKANI milioni 176. Mwaka 2010 ulikuwa mwaka wa kwanza wa TMAA kuendesha ukaguzi kwenye makampuni. Inawezekana kuwa madai kama haya yaliyokuzwa sana yamefanywa na makampuni mengine katika miaka iliyopita. Vilevile inawezekana kuwa madai yaliyokuzwa yalitolewa na sekta nyingine nje ya sekta ya madini.

Gharama za Motisha ya kodi.

Motisha ya kodi inamaanisha kuwa fedha ambazo zingekusanywa kama kodi hazikusanywi. Hii inamaanisha fedha pungufu katika hazina ya serikali. Hizi ni fedha ambazo zingetumika kugharamia bidhaa na gharama za umma katika bajeti ya maendeleo na ya matumizi ya kawaida. Hizi bidhaa na huduma hujumuisha pamoja na mengine miundo mbinu kama barabara na madaraja; huduma za jamii kama vile afya, elimu na maji. Gharama hizi zimeainishwa katika kisanduku kifuatacho.

Kisanduku 4: Baadhi ya gharama za motisha ya kodi
Maendeleo tuliyopoteza

Upunguzaji wa motisha ya kodi inayotolewa kwa makampuni kutawezesha upatikanaji wa rasilimali muhimu na kupunguza utegemezi kwa misaada ya nje. Endapo mapato yaliyopotea ya Shilingi za Tanzania 381 bilioni mwaka 2008/09 – 2009/10 yangetumika kwenye elimu na afya, bajeti ya elimu ingeongezeka kwa moja-ya-tano na bajeti ya afya kwa mbili-ya-tano.[55]

Uchambuzi zaidi kwenye Shilingi za Tanzania trilioni 1.02 zilizosamehewa mwaka 2011 inamaanisha kwa bajeti yote iliyopangwa kwa mwaka 2012/13, bajeti ya matumizi ya maendeleo na bajeti ya matumizi ya kawaida vilevile kwa fedha zilizopangwa kutoka kwa wahisani na ukopaji kwa ajili ya bajeti umeshafanywa, mwanzoni mwa taarifa hii. Yote haya yana maana kubwa na athari nyingi kwa mujibu wa maendeleo mengi tuliyoyapoteza. Kwa maana ya kiuchumi, misamaha hii ni gharama fursa tunayoingia kwa maana fedha zilizosamahewa haziwezekani tena wakati huo huo ziwepo kwa matumizi ya maendeleo kwa sababu mtu hawezi kuila keki yake na kuwa nayo.

55 IMF, Kenya, Uganda and United Republic of Tanzania: Selected Issues, 1 December 2006, p.10

8. Matatizo yanayotokana na Motisha ya Kodi

Shuhuda zote zinaonesha kwamba hasara za motisha za kodi zinazidi kwa mbali sana faida na ya kwamba motisha hizo hazihitajiki kuwavutia wawekezaji wa moja kwa moja wa nje(FDI).[56]

Watetezi wa motisha ya kodi mara nyingi hubisha kwamba udogo wa mzigo wa kodi unawapa wawekezaji kiwango halisi cha marejesho kilicho juu na kwa hivyo kuachilia huru ziada ya mapato kwa ajili ya kuwekeza tena. Kwa hiyo nchi mwenyeji inavutia ongezeko la wawekezaji wa moja kwa moja wa nje (FDI), inaongeza mapato yake pia inafaidi kutokana na uhamaji wa teknolojia. Hoja nyingine ya ubishani hasa kwa nchi zisizoendelea ni kwamba ni lazima kutoa motisha kwa wawekezaji kutokana na hali duni kimazingira kwa uwekezaji: Hali ya kisiasa isiyotabirika, miundombinu mbovu, gharama kubwa ya kuendesha biashara, hali ya uchumi mkuu usiyo imara, rushwa na udhaifu wa vyombo vya sheria. Upotevu wa mapato unahalalishwa na madai kwamba mtaji na nafasi za ajira zitakazotengenezwa zitaboresha hali ya maisha ya wananchi na kupanua uchumi.

Hata hivyo, kuna orodha ndefu ya hasara inayotokana na motisha ya kodi , kama ilivyoainishwa katika taarifa ya Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) inayodai zaidi ya mengine ya kwamba (motisha) hizo:

- Zinasababisha upotevu wa mapato yanayotokana na kodi ya sasa na ya wakati ujao
- Inajenga tofauti kati ya viwango vinavyofaa vya kodi na hivyo kuleta utata kati ya shughuli zilizopata ruzuku na zile ambazo hazikupata.
- Zinaweza kuhitaji rasilimali kubwa kiutawala au kiuendeshaji
- Zinaweza kupelekea hali ya utafutaji wa rushwa na shughuli nyingine zisizofaa.

56 Kuna maandishi mengi kuhusu madhumuni ya motisha za kodi. Tazama kwa mfano: There is M.Blomstrom, 'The Economics of International Tax Incentives', *http://www.oecd.org/dataoecd/55/1/2487874.pdf* and IMF, *Kenya, Uganda and United Republic of Tanzania: Selected Issues*, 1 December 2006

- Zinaweza, hasa kwa upande wa misamaha ya kodi ya mapato, kuwa njia isiyofaa katika kukuza uwekezaji. Makampuni yasiyopata faida katika miaka ya mwanzo ya uendeshaji, au makampuni kutoka nchi zilizoomba mkopo wa kodi ya nje ili kupunguza kodi ya nchi mwenyeji kutoka kwenye chanzo cha mapato ya nje, hazitanufaika kutokana na misamaha ya kodi ya mapato. Kinyume chake misamaha hiyo ina umuhimu kidogo kwa yale makampuni yanayoingiza faida tangu mwanzo wa uendeshaji wa shughuli zao.
- Zinaweza kuvutia makampuni yasiyo na msingi imara
- Zinaweza kuwa nje ya (mfumo) wa bajeti na kutokuwa na uwazi.[57]

Motisha za kodi zina mwelekeo wa kupunguza mapato ya serikali kwa kiwango cha asilimia 1 – 2 GDP (Zao Ghafi la Ndani) kwa mujibu wa OECD.[58] Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) unaainisha kuwa motisha za uwekezaji kama zinakusudiwa ziwe za manufaa, sharti zipangwe kwa umakini mkubwa na zilenge katika zile shughuli pekee zinazokusudiwa kukuzwa lakini " misamaha ya kodi ya mapato kwa makampuni makubwa " kwa kawaida hazifikii matakwa ya ulengaji makini wa motisha'.[59] Misamaha ya kodi zinapendelea zaidi uwekezaji wa mpito (muda mfupi) kuliko uwekezaji endelevu na hujenga fursa za wazi kwa ukwepaji hatari wa kodi.[60] Taarifa ya pamoja ya IMF, OECD, Shirika la Umoja wa Mataifa (UN) na Benki ya Dunia inafikia katika hitimisho hilo hilo, ikidokeza kwamba palipo na utawala dhaifu, misamaha ya kodi kwa makampuni makubwa ' kutaishia kufanya kidogo sana kuvutia uwekezaji' na hata ikivutia 'hii itakuwa ni kwa gharama au maumivu kwa uwekezaji wa ndani'.[61]

---

57 IMF, *Kenya, Uganda and United Republic of Tanzania: Selected Issues*, 1 December 2006, p.10

58 IMF, *Kenya, Uganda and United Republic of Tanzania: Selected Issues*, 1 December 2006, p.12

59 IMF, *Kenya, Uganda and United Republic of Tanzania: Selected Issues*, 1 December 2006,, p.16

60 World Bank, Foreign Investment Advisory Service, *Sector Study of the Effective Tax Burden in Tanzania*, May 2006, *http://siteresources.worldbank.org/EXTEXPCOMNET/Resources/2463593-1213973103977/09_Tanzania.pdf*

61 IMF, OECD, UN and World Bank, *Supporting the Development of More Effective Tax Systems*, Report to the G-20 Development Working Group, 2011, p.19

Utumiaji wa kanuni na taratibu zinazotofautiana hufanya utawala wa shughuli za kodi kuwa mgumu na huongeza gharama, wakati huo huo husababisha gharama za kijamii zinazotokana na ufisadi na rushwa pale ambapo kanuni za utoaji wa misamaha ya kodi zinapokiukwa, kama inavyotokea mara kwa mara.[62] Motisha za kodi pia zinaweza kutumika vibaya pale ambapo motisha husika imeisha na wakuza biashara (wawekezaji) kwa hila hufunga biashara husika na wakati huo huo huanzisha chombo kingine kipatiwe motisha zile zile za kodi. Motisha za kodi vile vile huelekea kupendelea wawekezaji binafsi wenye ujuzi ambao kwa kweli wana mitaji yao binafsi ya kutosheleza.[63] Zaidi ya hayo, mara motisha zinapotolewa kwa waliochaguliwa, sekta zile zinazojiona kuwa zimeachwa zitajitahidi kudai kuwa miongoni mwa hao na hivyo kupanua wigo wa motisha zaidi. Mara motisha zinapotolewa ni vigumu sana kisiasa kuziondoa. Kwa baadhi, motisha ni upotevu wa ziada wa rasilimali kwa maana makampuni mengi yangeweza kuwekeza bila hata ya motisha yoyote. Kwa ujumla, motisha za uwekezaji zinapendekezwa ikiwa biashara iko katika asili ya kutoa bidhaa yenye manufaa au huduma kwa umma, kama vile teknolojia ya kusaidia kulinda mazingira huduma ya afya ya msingi, na uzuiaji wa magonjwa, kukuza ujuzi wa wafanyakazi, utafiti na maendeleo.[64]

Motisha za Kodi na Wawekezaji wa Nje wa Moja kwa Moja

Tafiti zilizofanywa ….zinaonesha kuwa 'uwekezaji uliovutiwa na kodi huwa hautoi chanzo imara ya uwekezaji katika nchi inayopokea

62 H.Zee at al, 'Tax Incentives for Business Investment: A Primer for Policy Makers in Developing Countries', *World Development*, Vol. 30, No. 9, 2002, pp. 1497-1516.

63 Goldin and Reinert, 'Globalization for Development, Trade, Finance, Aid, Migration and Policy, 2007; wakizungumzia pia utafiti wa Benki ya Dunia wa mwaka1998 World Bank study, the authors argue that poor people face higher tariffs than the non-poor by more than twice. Poor people also face significant tariff peaks in products of export interest to them.

64 Mada iliyotolewa na Timu ya Kurahisisha Kodi za Kimataifa ya IFC, Ushauri wa Mazingira ya Uwekezaji Katika Warsha ya EAC kuhusu Kuhtibitisha Utafiti wa Mbinu (Modeli) ya Kuondokana na Hali ya Ulipaji wa Kodi Maradufu na Kanuni /Nidhamu Dhidi ya Ushindani Mbaya wa Kodi iliyofanyika Arusha, Aprili 2011.

wawekezaji' (Taarifa ya Pamoja ya IMF, OECD, UN na Benki ya Dunia kwa kundi G-20)[65]

Ushahidi unaonesha kuwa motisha za kodi hazihitajiki kuvutia Uwekezaji wa moja kwa moja wa Nje (FDI). Taarifa ya mwaka 2006 iliyotolewa na Idara ya Afrika ya IMF, ikijikita katika motisha za kodi katika Afrika ya Mashariki, inainisha kuwa hasara zilizosababishwa na motisha za kodi kama ilivyoorodheshwa (katika aya zilizopita) hapo juu: Inaungwa mkono na ushahidi wa takwimu zilizopo ambazo zinathibitisha kuwa motisha za uwekezaji hasa motisha za kodi siyo jambo muhimu kuvutia uwekezaji wa nje.[66]

Taarifa ya IMF inadai kuwa nchi zilizofanikiwa sana katika kuwavutia wawekezaji wa nje hazikutoa motisha kubwa ya kodi au motisha zingine. Utoaji wa motisha hizo hakutoshi kuvutia uwekezaji mkubwa wa nje ikiwa mambo mengine hayapo mahali pake. Taarifa hiyo pia inainisha kuwa ` katika mazingira maalum' motisha za uwekezaji zilizolengwa kwa umakini ni sababu mojawapo yenye kuathiri / gusa maamuzi ya uwekezaji' lakini `mwishoni' motisha za uwekezaji ni nadra kutokea kuwa jambo la muhimu sana katika maamuzi ya uwekezaji'.[67] Hitimisho hili linaungwa mkono na maandishi mengi yanayoonesha kuwa mambo muhimu zaidi katika kuvutia Uwekezaji moja kwa moja wa Nje (FDI) ni ubora wa miundo mbinu, gharama ndogo ya uanzishaji na uendeshaji wa biashara, utulivu wa kisiasa, na sera ya uchumi mkuu inayotabirika.[68] Hakika, hii mantiki kwa sehemu inaeleza kwa nini IMF na mashirika mengine ya kimataifa kama vile Benki ya Maendeleo ya

65 *IMF, Kenya ,Uganda and United Republic of Tanzania: Selected Issues*, 1 December 2006, p.11

66 IMF, *Kenya, Uganda and United Republic of Tanzania: Selected Issues*, 1 December 2006, p.11

67 IMF, *Kenya, Uganda and United Republic of Tanzania: Selected Issues*, 1 December 2006, p.11

68 Katika mazungumzo ya pamoja ya Mtandao wa Haki za Biashara-Afrika/Action Aid (Trade Justice Network-Africa/ActionAid) uliofanyika Nairobi Julai 2011, John Njiraini, Kamishna wa Kodi ya Ndani Kenya, alithibitisha huu ukweli. Alitoa mfano, wa mlipa kodi mkubwa , kampuni ya Blue Chips Kenya iliyoongeza kiwango cha uwekezaji kwa kiasi kikubwa miezi michache baada ya Mamlaka ya Mapato Kenya (KRA) kuondoa baadhi ya motisha zilizokuwapo awali. Inavyoonekana aina fulani ya wawekezaji , wengi wao wakiwa wakubwa waliruhusiwa kupunguza kodi ya ongezeko la thamani dhidi ya dhima zingine za kodi, chombo kilichoondolewa kutokana na changamoto katika usimamizi wake.

Afrika, wamekuwa wakitaka serikali ya Tanzania, na serikali nyingine za Afrika ya Mashariki, kupunguza sana misamaha ya kodi. (tazama kipengele cha 4).

Katika Tanzania, uanzishaji wa EPZs mwaka 2002 'haujaleta ongezeko linaloonekana katika uwekezaji wa nje', taarifa ya IMF ya mwaka 2006 yaainisha. Uganda imeendelea kuvutia viwango vya juu vya uwekezaji wa moja kwa moja wa nje (FDI) kuliko Tanzania ambayo hutoa motisha kubwa zaidi za uwekezaji.[69] Kiwango kikubwa cha motisha za kodi zinayotolewa Zanzibar zinakusudiwa kuvutia Uwekezaji wa moja kwa moja wa Nje (FDI), hata hivyo mtiririko wa uwekezaji wa moja kwa moja wa nje (FDI) ni mara chache sana kuzidi DOLA ZA KIMAREKANI milioni 19 katika mwaka mmoja.[70] Jedwali linalofuata linaonesha kuwa wakati Tanzania imepokea kwa kiwango kikubwa mtiririko wa FDI katika miaka ya karibuni, kumekuwa na ongezeko dogo sana katika mtiririko wa FDI katika miaka mitano 2006-10 –ya kiasi cha zaidi kidogo tu cha DOLA ZA KIMAREKANI milioni 100. Uganda imepokea mtiririko mkubwa zaidi wa FDI katika kanda hii ambao umekuwa ukiongezeka. Katika Kenya, ambayo hutoa kiwango kikubwa cha motisha ya kodi, FDI ni mdogo tena hautabiriki.[71]

Jarida Na 6: Mtiririko wa Uwekezaji wa Nje (FDI) Nchini Tanzania, Kenya na Uganda (Dola ya Marekani milioni)

	2006	2007	2008	2009	2010
Kenya	51	729	96	141	133
Tanzania	597	647	679	645	700
Uganda	644	792	729	816	848

Chanzo: UNCTAD,UNCTAD, *World Investment Report 2011*, Annex Table1.1

Ukubwa wa Uwekezaji wa Nje (FDI) Tanzania

Taarifa iliyopo ya hivi karibuni kuhusu uwekezaji Tanzania (BoT, NBS na TIC, 2009: vii) inaonesha kuwa hisa dhamana ya Uwekezaji wa

69 IMF, *Kenya, Uganda and United Republic of Tanzania: Selected Issues*, 1 December 2006, p.13

70 'Zanzibar Investment Policy', *http://www.zanzibarinvest.org*, p.2.

71 Uganda Investment Authority: 'Why invest in Uganda?', *http://www.ugandainvest.go.ug*

moja kwa moja wa Nje (FDI) uliendelea kuongezeka kutoka DOLA ZA KIMAREKANI milioni 4,438.7 mwaka 2005 hadi DOLA ZA KIMAREKANI milioni 6,239.9 mwaka 2008. Hili ni ongezeko la asilimia 40.6 katika kipindi husika. Kwa mujibu wa IMF (2011), thamani ya Uwekezaji wa Nje (FDI) katika Tanzania (kiasi halisi kilichopo cha sasa katika DOLA ZA KIMAREKANI) kilikuwa dola za kimarekani 433,441,900[72]. Gazeti la 'The Citizen[73], ikinukuu UNCTAD (2011) inaarifu kuwa ingawa kuna hali ya kushuka kwa FDIs tangu mwaka 2008 kufuatia mdororo wa kiuchumi, Tanzania imeonesha ongezeko la 8.5% katika FDIs mwaka 2010. Mtiririko (wa FDIs) uliongezeka kutoka DOLA ZA KIMAREKANI milioni 645 mwaka 2009 hadi dola za kimarekani milioni 700 million mwaka 2010.

Makala mbalimbali ya Taarifa ya Uwekezaji Tanzania zinabainisha kuwa Uwekezaji wa wa moja kwa moja wa Nje (FDIs) umekuwa ukitiririka katika karibu kila sekta za uchumi na maeneo mengi ya kijiografia tangu katikati ya miaka ya 1980-89. Kwa mfano hisa dhamana ya FDIs (katika milioni ya Dola za Marekani -DOLA ZA KIMAREKANI) kwa kipindi cha 2005 – 2008 ilikuwa 4,438.7 kwa 2005 wakati kwa mwaka 2006 ilikuwa 4,827.1. kwa miaka ya 2007 na 2008[74] hisa dhamana ilikuwa 5,950 na 6,239.9 kwa mfuatano[75]. Kwa upande wa usambazaji wa kijiografia wa FDIs hisa dhamana kwa kipindi hicho hicho, jumla ya mikoa 16 ya Tanzania Bara ilipata kiasi fulani ya hisa dhamana ya FDIs. Mkoa wa Dar es Salaam ndiyo uliokuwa na hisa nyingi (58%) ukifuatiwa na Shinyanga (12.3%), Mwanza (9.7%) na Arusha (5.7%). Hisa dhamana iliyokuwa ndogo sana ilikuwa ya mkoa wa Pwani ikiwa na 0.1% ya jumla ya hisa dhamana za FDI kwa nchi nzima.[76]

Mashindano ya Mbio za kuelekea Chini.

Motisha za kifedha zinazowekwa katika nchi moja zinaweza kupelekea katika mashindano ya kodi miongoni mwa nchi na hatimaye 'mbio za kuelekea chini' hali ambayo inashuhudiwa katika Afrika ya Mashariki. Mashindano ya kodi yanaweza kutokea pale ambapo makampuni

72 IMF Balance of Payment Statistics Year Boos 2011, online at *http://www.indexmundi.com/facts/tanzania/foreign-direct-investment*

73 Online at *http://thecitizen.co.tz/news/51-other-news/13184-fdi-inflows-into-tanzania-increase-85pc-to-hit-700m.html* (retrieved on 16th March 2012)

74 Provisional

75 See BoT, NBS and TIC (2009:21) for details

76 See BoT, NBS and TIC (2009:25) for details

yanaweza kung'amua sehemu ambapo viwango vya kodi ni vidogo zaidi, na hivyo kupelekea nchi nyingine kushusha viwango vyao vya kodi ili kuvutia na kubakisha makampuni yenye nguvu na wafanyakazi wenye uwezo.[77] Mashindano ya kodi huleta ugumu katika kuzifanya nchi kudumisha viwango vya kodi vinavyotakiwa, na kupelekea katika ushukaji endelevu wa viwango vya kodi na mapato. Kwa nchi zote mbili Kenya na Uganda, kwa mfano, serikali zinatoa motisha nyingi sana za kodi, kwa sehemu ni katika mashindano ya kuvutia na kubakisha FDIs, matokeo yake ni upotevu mkubwa wa mapato ya serikali, kama ilivyo kwa Tanzania. Tofauti katika viwango vya kodi katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki zimepelekea katika biashara haramu, ugumu katika mifumo ya uendeshaji kwa makampuni yanayopenda kufanya biashara kote katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na hivyo kupunguza kasi ya mfungamano.

Mawaziri wa Fedha na Uchumi wa Umoja wa nchi za Ulaya (EU) wametafsiri ushindani wa kodi wenye madhara kuwa ni ule unaojumuisha kama vile: kiwango cha kodi kilichopo ambacho ni kidogo sana kuliko kiwango cha kawaida cha kodi katika nchi husika; uwepo wa aina za unufaikaji wa kodi zilizotengwa kwa ajili ya wageni; na motisha za kodi kwa shughuli ambazo zimetengwa kutoka katika uchumi wa ndani na kwa hiyo hazina matokeo chanya kwenye misingi ya kodi ya Taifa.[78]

Jumuiya ya Afrika ya Mashariki imechukua hatua madhubuti kupanua na kuongeza kina cha ushirikiano wa kiuchumi miongoni mwa wanachama wake. Kifungu cha 83 cha mkataba unaounda Jumuiya ya Afrika ya Mashariki una kipengele kinachohusu maafikiano ya kifedha na hazina ikiwa ni pamoja na uondoaji wa tofauti katika kodi. Vizuizi vya ushuru kati ya Kenya, Uganda na Tanzania, nchi wanachama wa awali katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, viliondolewa mwaka 1999. Rwanda and Burundi walijiunga na Jumuiya mwaka 2007.[79] Hata hivyo Tanzania pamoja na nchi wanachama wa Jumuiya, inachukua hatua ndogo sana kuimarisha huu uratibu wa kifedha Afisa wa ngazi ya juu wa Kituo cha

77 A.Hansson and K.Olofsdotter,'Integration and Tax Competition: An Empirical Study for OECD Countries', econpapers.repec.org/RePEc:hha:lunewp:2005_004

78 Petersen et al, 'Tax Systems and Tax Harmonization in the East African Community (EAC)', p. 22, *http://www.eacgermany.org/index.php/documents-and-studies/cat_view/39-tax-harmonisation-in-the-eac/43-study-on-tax-systems-in-the-eac*

79 'About EAC', *http://www.eac.int/about-eac.html*

Uwekezaji Tanzania (TIC) aliwajulisha watayarishaji wa chapisho hili kwamba ni lazima kuwe na tathmini endelevu ya mpango uliokubalika kuhusu maafikiano ya mfumo wa kodi baina ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ili kukabili changamoto za athari ya mashindano ya ya kodi.

Msingi Finyu wa mapato ya Kodi Tanzania

Upunguzaji wa motisha za kodi kutapanua msingi wa mapato ya kodi Tanzania, ambao hivi sasa ni mfinyu. Kwa mujibu wa taarifa ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ya mwaka 2008. Walipa kodi wakubwa 39 walichangia kiasi cha 80% ya mapato ya Tanzania yanayotokana na kodi.[80]. Wigo mpana msingi wa kulipa mapato ya kodi, hatimaye utapunguza baadhi ya viwango vya kodi na kushawishi wakwepa kodi.[81]. Sekta isiyo rasmi inachangia kati ya aslimia 40 and 60 ya Zao ghafi la Ndani (GDP)[82] na karibu asilimia 70 ya nguvu kazi ya Tanzania[83] lakini isiyotozwa kodi. Idadi ya watu wanaolipa kodi Tanzania ni ndogo: Kwa mujibu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ni watu milioni 1.6 tu kati ya watu milioni 15 wenye uwezo wa kulipa kodi.[84]

---

80 African Development Bank, *Domestic Resource Mobilisation for Poverty Reduction in East Africa: Tanzania Case Study*, November 2010, p.21

81 Sawasawa na wanachama wenzake wa EAC, serikali inachukua hatua za kupanua wigo wa kodi kwa kujumuisha sekta isiyo rasmi. Afisa wa Ngazi ya Juu wa Wizara ya Fedha alisema kuwa kupanua mzigo wa kodi kutafanya mfumo wa kodi kuwa wa usawa zaidi na hilo lifanyike ili kuhakikisha kuwa urasimishaji wa sekta isiyo rasmi hakutakuwa kama adhabu wala wa gharama kubwa. A. Elinaza, 'TRA Eye Now Turns to Informal Sector to Fill Tax Collection Gap', www.allafrica.com, 6 December 2010

82 Ukubwa wa uchumi usio rasmi kwa kutafsiri ni vigumu kukisia. Serikali na Asasi ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii (Economic and Social Research Foundation) wanakadiria kuwa 40%. (TRA, *Review of Informal Sector for Taxation Purposes*, Draft, January 2011, p.xii; 'Informal Sector Taxation in Tanzania', *TAKNET Policy Brief, No.12*, 2010, p.1); A recent World Bank analysis suggests around 60 per cent (Friedrich Schneider et al, *Shadow Economies all over the World: New Estimates for 162 Countries for 1999 to 2007*, World Bank, June 2010); the Tax Justice Network has recently used a figure of 56.3 per cent (*The Cost of Tax Abuse: A Briefing Paper on the Cost of Tax Evasion Worldwide*, November 2011)

83 'TRA has no tax evasion statistics', *Daily News*, 11 August 2010

84 'Tax compliance is a legal obligation', *Daily News*, 12 December 2011, citing a recent TRA report

Kiashirio kingine cha msingi finyu wa kodi Tanzania ni makusanyo kama sehemu ya Zao ghafi la ndani (GDP). Hii inaonekana katika taarifa ya Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) inayooneshwa hapa chini:

Jedwali 7: Mapato ya Ndani Kama Asilimia ya Zao Ghafi la Ndani (GDP) (makusanyo halisi)[85]

2005/06	2006/07	2007/08	2008/09	2009/10
11.4	13.0	14.7	15.3	14.6

Kutokana na jedwali hapo juu, inaonekana kwamba makusanyo ya kodi yamekuwa karibu asilimia 15 ya Zao ghafi la ndani (GDP). Mlinganisho wake kwa Kenya ni asilimia 19 na kwa Uganda ni asilimia 11.8.[86] Katika nchi za OECD, kiwango mlingano ni karibu asilimia 30.[87]

Kwa mujibu wa Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF), Tanzania ina uwezo wa mapato ya kodi ya asilimia 20.9 ya Zao ghafi la Ndani (GDP)[88]. Kwa makusanyo halisi ya asilimia 15 , ina maana kwamba pengo la kodi (tofauti kati ya makusanyo halisi na makusanyo yaliyopo – yanayoweza kukusanywa)[89] ni kiasi cha asilimia 6 ya Zao ghafi la Ndani (GDP)

85 IMF, *Staff Report for the 2011 Article IV Consultation and Second Review under the Policy Support Instrument*, 21 April 2011, p.25; World Bank, *United Republic of Tanzania, Public Expenditure Review 2010*, September 2011, pp.9, 85. Government figures on no and non-tax revenues show collections of 16.4 per cent of GDP in 2009/10 and a projection of 16.1 per cent of GDP in 2010/11. MOF, *Budget Digest 2010/11*, June 2010, unpaginated, section III; Tanzania, memorandum to the IMF, 15 April 2011, in IMF, *Staff Report for the 2011 Article IV Consultation and Second Review under the Policy Support Instrument*, 21 April 2011, p.37

86 IMF, *First Review under the Three-Year Arrangement under the Extended Credit Facility*, 15 June 2011, p.20

87 Nehemiah Osoro, *Domestic Resource Mobilisation in Sub-Saharan Africa: The Case of Tanzania*, 2010

88 IMF, *Seventh Review under the Policy Support Instrument*, 18 May 2010, p.20

89 This IMF analysis does not define what it means as the 'tax gap'. We understand it refers to uncollected revenues from the informal sector and also from tax exemptions. The 'tax gap' is usually referred as 'the difference between what is legally due under the law, and what the government will be able to collect' (IMF Task Force on Harmonization of Public Sector Accounting—Working Group 2, July, 2004, *http://www.imf.org/external/np/sta/tfhpsa/2004/trjd.pdf*

9. Sera ya Serikali Kuhusu Motisha ya Kodi

Serikali inatambua kuwa misamaha ya kodi inasababisha upotevu mkubwa wa mapato na inachukua hatua kadhaa kupunguza hali hiyo. Hata hatua ni za kusuasua na kiwango halisi cha umakini wa serikali unatia mashaka. La muhimu zaidi kwa uchambuzi huu, ni kuwa bado haieleweki vizuri serikali itachukua hatua zipi zaidi kupunguza motisha za kodi zilizotolewa kwa makampuni ya madini na biashara zinazoendeshwa katika maeneo tengevu ya EPZs na SEZs.

Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko alisema, kwa mfano, kwamba 'nchi nyingine zote zinatoa motisha za aina hii (kwenye EPZ) …..kama hatukuamua kutoa, hakuna mwekezaji ambaye angelikuja.'[90] Mpango wa EPZ wa Tanzania umevutia uwekezaji wenye thamani ya dola za kimarekani milioni 569 katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, umetengeneza ajira 10,500, kwa mujibu wa Afisa wa Ngazi ya Juu wa EPZA .[91] Hii ina maana kwamba kila nafasi ya ajira imegharimu kiasi cha DOLA ZA KIMAREKANI milioni 54,000 (Shilingi za Tanzania milioni 92) kutengenezwa – kiwango kikubwa kweli. Ni muhimu pia kutambua kuwa ubora wa ajira iliyotengenezwa lazima unazingatiwa ili kuhalalisha motisha. Kadiri kunavyokuwa na nafasi nyingi za kazi zenye kuhitaji ujuzi wa juu, malipo bora na ya kudumu kwa Watanzania, kwa kulinganisha na jumla ya nafasi zilizopo ndivyo inavyokuwa bora kwa nchi. Hata hivyo nafasi ya ajira pekee bila uzingatiaji wa vigezo vilivyotajwa hapo juu haitoshi kuhalalisha motisha.

Hata IMF, mwungaji mkono wa siku nyingi wa kodi ndogo, sasa hivi inahimiza serikali kupandisha kodi kwa makampuni ya uchimbaji madini. Imeshauri kuwe na kodi ya zuio katika riba inayolipwa kwenye mikopo ya fedha za kigeni; ukomo katika makato ya malipo ya madeni ya kodi ya mapato; na kupunguza motisha zinazotolewa katika posho za uwekezaji kwa ajili ya utafiti na maendeleo.[92] Mnamo Mei

90 See, 'EPZ, SEZ Programmes come under one Regulator', *http://www.epza.co.tz*

91 Victor Karega, '10,500 jobs created from investing $569m in EPZs', *The Citizen*, 14 April 2011

92 IMF, *Seventh Review under the Policy Support Instrument*, 18 May 2010, p.20

2011 aliyekuwa Naibu wa Waziri wa Nishati na Madini Adam Malima, alinukuliwa akisema kwamba serikali 'itapangua mpango mzima unaohusu misamaha ya kodi' kwa ajili ya makampuni ya uchimbaji madini.[93] Hata hivyo, ahadi hii bado haijatekelezwa.

Kuhusu misamaha ya kodi kwa upana zaidi, aliyekuwa Waziri wa Fedha Mustafa Mkulo, alisema katika hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2011/12 kwamba serikali imeshaanza kuchukua hatua ' kupitia taratibu za misamaha ya kodi ili kuimarisha udhibiti juu ya ukiukaji na ya kwamba sera ya serikali ni kupitia na kuzisawazisha sheria mbalimbali za kodi, zenye vifungu vya misamaha kwa lengo la kupunguza misamaha hiyo. Alisema sera ya serikali ni kupunguza misamaha kutoka kiwango kilichopo cha asilimia 2.5 ya GDP katika makisio yake mpaka angalau asilimia 1 ya GDP'.[94] Hii ni katika kutambua ukweli kwamba

> '*Viwango vinavyoongezeka vya msamaha wa kodi vinachangia katika ukusanyaji mdogo wa mapato, na hivyo kudhoofisha uwezo wa serikali kugharamia mahitaji ya jamii kiuchumi na kimiundombinu na hatimaye kupunguza kasi ya kuimarisha maisha ya watu. Misamaha ya kodi pia imejenga mianya ya ukwepaji wa kodi na uvujaji wa mapato*.[95]

Katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2009/2010 aliyekuwa wakati huo Waziri wa Fedha alisema kuwa serikali imependekeza kutengua matangazo ya serikali 405 yenye kutoa misamaha ya kodi kwa makampuni binafsi, mashirika yasiyo ya serikali, mashirika ya kidini, mashirika ya kimataifa na miradi ya serikali iliyokamilika ili kuzuia mmomonyoko wa mapato ya kodi. Waziri alisema kuwa matangazo ya serikali mengi yaliyotolewa katika kipindi cha 1964-2005 hayako wazi na hayabainishi ni aina gani ya kodi inayosamehewa, na mapatano ya msamaha ni kiasi gani. Alipendekeza hatua kama vile kutengua Tangazo la Serikali Na. 99 of 2005 kuhusu msamaha wa sehemu ya ushuru wa mafuta na pia ushuru wa ndani uliotolewa kwa makampuni ya uchimbaji madini.[96] Kwa bahati mbaya, ni hatua chache sana ambazo zimechukuliwa hadi sasa. Siyo misamaha yote iliyoorodheshwa na Waziri katika hotuba yake ya bajeti

93 Ally Hamisi, 'Tanzania asked to raise mining tax', *East Africa Business Week*, 16 May 2011

94 Finance Minister, Budget Speech 2011/12, pp.11, 25, www.mof.go.tz

95 Finance Minister, Budget Speech 2009/2010, paras. 78, 71, www.mof.go.tz

96 Finance Minister, Budget Speech 2009/2010, para. 78, www.mof.go.tz

ya mwaka 2009/2010 – hasa ile inayonufaisha makampuni ya madini – imetenguliwa, ingawaje baadhi ya misamaha kwenye kiwango cha ushuru wa ndani kwa mfano, imetenguliwa.

Taarifa ya pamoja ya Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na IMF, inasema kuwa serikali inasua sua sana katika kupunguza misamaha ya kodi. AfDB inabaini 'upinzani endelevu kutoka kwa tabaka la watu wenye uwezo katika rai ya kufuta misamaha mikubwa ya kodi iliyopo sasa hivi.[97] Wote wawili, AfDB na IMF wanaisihi Tanzania kupunguza kwa kiwango kikubwa misamaha ya kodi.

Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) inaainisha kwamba:

> '*Kiwango cha misamaha siyo tu imechangia katika kuhujumu ufanisi na upatikanaji wa pato bayana yanayotokana na marekebisho yaliyotokea kiutawala, lakini pia kwenye upotevu mkubwa wa mapato, yumkini inayopelekea kwa kiwango kikubwa pengo la kodi nchini Tanzania*.[98]

Katika taarifa ya Aprili 2011, IMF ilisema kwamba 'misamaha imeongezeka kupita mipaka, hasa ya thamani ya ongezeko la bidhaa (VAT); na ingeweza kupunguzwa kwa manufaa'. Hata hivyo mamlaka zote zimesema kuwa wana taarifa kuhusu suala hilo lakini waliingia katika matatizo ya kisiasa walipojaribu kupunguza misamaha'. Kwa hiyo walikuwa wanaachia jukumu hilo kwenye marekebisho ya usimamizi wa kodi. Katika taaarifa yake ya Aprili 2011 kwa IMF, serikali iliarifu IMF kwamba itafanya 'utafiti makini, kuhusu upeo wa upunguzaji misamaha ya kodi na ya kwamba ' itaimarisha tu usimamizi na udhibiti wa misamaha ya kodi'.[99]

97 African Development Bank, *Domestic Resource Mobilisation for Poverty Reduction in East Africa: Tanzania Case Study*, November 2010, p.vi

98 African Development Bank, *Domestic Resource Mobilisation for Poverty Reduction in East Africa: Tanzania Case Study*, November 2010, p.21

99 IMF, *Staff Report for the 2011 Article IV Consultation and Second Review under the Policy Support Instrument*, 21 April 2011, pp. 17, 41

10. Mapendekezo

Kwa mtazamo wetu, serikali inapaswa:

- Kuondoa motisha zinazotolewa ili kuvutia na kubakisha FDIs hasa zile zinazotolewa kwa sekta za uchimbaji madini, EPZs na SEZs.
- Kuendesha utafiti huru ili kutathmini faida za kiuchumi na kiasi cha mapato ya kigeni yaliyopatikana kutoka maeneo ya EPZs na SEZs kwa kulinganisha na motisha zilizotolewa na serikali
- Kufanya mapitio, yatakayowekwa wazi kwa umma, kuhusu motisha za kodi zote kwa lengo la kupunguza au kuondoa nyingi ya hizo, hasa zile zinatolewa na Mawaziri kwa mamlaka walizopewa. Motisha zitakazobaki lazima ziwe rahisi kuziendesha na kuzisimamia na serikali ioneshe zina manufaa kiuchumi.
- Kutoa kila mwaka, wakati wa uandaaji wa bajeti, taarifa ya wazi kwa umma yenye kuonesha mchanganuo wa matumizi ya kodi, pia ikionesha takwimu za mwaka juu ya gharama za serikali kutokana na motisha za kodi na wanaonufaika na misamaha hiyo.
- Kuweka mfumo ulio wazi wa majukumu na uwajibikaji wa serikali kwa wananchi kuhusu masuala ya motisha za kodi katika ngazi zote za serikali.
- Kuimarisha uratibu katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ili kuchukua hatua dhidi ya ushindani wenye madhara katika utoaji wa motisha za kodi. Hii inamaanisha kukubaliana katika uondoaji wa motisha zote za kodi zenye kuhusu FDIs. Hii haimaanishi kufikia kwa ukamilifu *maafikiano* ya kodi katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) bali kuongeza *uratibu,* na kuruhusu nchi binafsi mnyumbuliko kifedha. Kwa upande mwingine, hii kimsingi ina maana ya kuboresha rasimu iliyopo ya Kanuni ya Uendeshaji wa Ushindani wa Kodi katika EAC, na kukubaliana:

    - *Viwango vya chini* kwenye kodi fulani fulani, kukwepa athari ya ushindani wa kodi.
    - Kuweka utaratibu wa kisheria wa kupeana taarifa za mara kwa mara kwa nchi nyingine kuhusu mabadiliko yanayopendekezwa katika viwango vya kodi
    - Kuzingatia viwango vya juu vya uwazi, Kama vile Kanuni Bora za Utendaji Katika Uwazi wa Kifedha za IMF (zinavyoainisha).

- Kuunda chombo madhubuti cha kusuluhisha migogoro.
- Kuandaa kila mwaka uchambuzi wa matumizi ya kodi zinazoweza kulinganishwa na kuwekwa wazi kwa umma.

Mapendekezo mengine muhimu ni kama yalivyoainishwa katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu (CAG) ya mwaka 2011. Baadhi yake zinafanana na zilizopo hapo juu. Hizi zinajumuisha:

i) Sheria ya kodi kuhusu misamaha ifanyiwe mapitio ili kufanyia kazi na kuboresha vyanzo vya kodi.
ii) Serikali ama iweke ukomo wa misamaha kwenye 5% ya jumla ya makusanyo ya mapato au iache kabisa utoaji wa misamaha ya kodi zinazonufaisha watu wenye uwezo na makampuni ambao wanapaswa kulipa kodi.
iii) Motisha za kodi zinazotolewa na TIC zifutwe au kuwe na maafikiano na TRA na wakala wengine wa serikali.
iv) Kuna haja ya utafiti kufanyika kuona ni kiasi gani nchi inakusanya kutoka kwa wawekezaji na inapoteza kiasi gani kutokana na misamaha ya kodi.
v) Serikali inapaswa kufanya mapitio ya sera yake ya misamaha ya kodi kwa lengo la kupunguza viwango vya misamaha ya kodi. Kuna haja ya kuhakikisha kwamba kiasi cha misamaha inayotolewa kinawekewa kiwango cha chini kinachoweza kuvumilika na ni ya lazima kwa maslahi ya umma.
vi) Serikali haina budi kudhibiti mianya ya kodi pamoja na misamaha ya kodi na uhamishaji haramu wa bei miongoni mwa makampuni makubwa ya kimataifa.

Taasisi Zilizohojiwa

Muungano wa Viwanda Tanzania (Confederation of Tanzania Industries)
Chuo cha Benki Tanzania (The Tanzania Institute of Bankers)
Wizara ya Fedha (Ministry of Finance)
Kituo cha Uwekezaji Tanzania (Tanzania Investment Centre)
Benki ya Afrika (Bank of Africa)
Chuo cha Usimamizi wa Fedha (Institute of Finance Management)
Umoja wa Nchi za Ulaya (European Union)
Bodi ya Rufaa ya Mapato ya Kodi (Tax Revenue Appeals Board)
Mamlaka ya Mapato Tanzania (Tanzania Revenue Authority)
Shule ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (University of Dar es Salaam School of Business)
Mamlaka ya Mapato Zanzibar (Zanzibar Revenue Authority)
Mamlaka ya Ukuzaji wa Uwekezaji Zanzibar (Zanzibar Investment Promotion Authority)

Marejeo.

Ally Hamisi, 'Tanzania asked to raise mining tax', East Africa Business Week, 16 May 2011

African Development Bank, Domestic Resource Mobilisation for Poverty Reduction in East Africa: Tanzania Case Study, November 2010

BoT, NBS and TIC (2009): Tanzania Investment Report 2009

Controller and Auditor General (CAG) 2010/2011 Annual General Report of the Controllerand Auditor Generalon the auditof public authorities and otherbodies for the financial year 2010/2011

Controller and Auditor General (CAG) annual general report on the Audit of the Financial Statements of the Central Government for the Year Ended 30th June, 2011

Global Tax Simplification Team of the IFC Investment Climate Advisory (April, 2011): Study of Double Taxation Avoidance Model and the Code of Conduct Against Harmful Tax Competition, Arusha, April 2011

Goldin and Reinert, 'Globalization for Development, Trade, Finance, Aid, Migration and Policy, 2007

H. Zee at al, 'Tax Incentives for Business Investment: A Primer for Policy Makers in Developing Countries', World Development, Vol. 30, No. 9, 2002

IMF, Staff Report for the 2011 Article IV Consultation and Second Review under the Policy Support Instrument, 21 April 2011

IMF, Seventh Review under the Policy Support Instrument, 18 May 2010

IMF, Kenya, Uganda and United Republic of Tanzania: Selected Issues, 1 December 2006

IMF, OECD, UN and World Bank, Supporting the Development of More Effective Tax Systems, Report to the G-20 Development Working Group, 2011

IMF, First Review under the Three-Year Arrangement under the Extended Credit Facility, 15 June 2011

Mark Curtis and Tundu Lissu, A Golden Opportunity: How Tanzania is Failing to Benefit from Gold Mining, October 2008

MOF, Financial Statement and Revenue Estimates, 2011/12 Budget, Vote 21, www.mof.go.tz

Nehemiah Osoro, Domestic Resource Mobilisation in Sub-Saharan Africa: The Case of Tanzania, 2010

Odd-Helge Fjeldstad and Kari Heggstad, 'Tax system in Tanzania: Capacity and Constraints',

Policy Forum, 'How Much Revenue Are We Losing?', Policy Brief, March 2009

PKF, Tanzanian Tax Guide 2010

Tanzania Export Processing Zones Authority and the Export Processing

Zones Act No. 11 of 2002

The Citizen, 4th April 2012

The Citizen, 26 June 2011

TMAA, Annual Report 2010

TRA, Taxes and Duties at a Glance 2010/2011

Uwazi, 'Tanzania's Tax Exemptions: Are they too high and making us too dependent on Foreign Aid?', Policy Brief, TZ.12/2010E

World Bank, United Republic of Tanzania, Public Expenditure Review 2010, September 2011

Vyanzo vya Tovuti

http://www.businessdictionary.com/definition/tax-incentive.html accessed on 11th April, 2011.

A .Hansson and K.Olofsdotter, 'Integration and Tax Competition: An Empirical Study for OECD Countries', econpapers.repec.org/RePEc:hha:lunewp:2005_004

David Malingha Doya, 'Tanzania May Abolish Tax Refund for Miners to Boost Revenue', 25 October 2011, www.bloomberg.com

EAC, online at *http://www.eac.int/about-eac.html*

Finance Minister, Budget Speech 2011/12, p.25; Budget Speech

2009/2010, para. 78, http://www.mof.go.tz

'Corporate Tanzania: Business, Trade and Investment Guide 2010/2011', *www.corporate-tanzania.com*, p.57; Tanzania Investment Centre, 'FAQ Related to Investing in Tanzania'http://www.tic.co.tz/

IMF Balance of Payment Statistics Year Boos 2011, online at *http://www.indexmundi.com/facts/tanzania/foreign-direct-investment*

IMF Task Force on Harmonization of Public Sector Accounting—Working Group 2, July, 2004, http://www.imf.org/external/np/sta/tfhpsa/2004/trjd.pdf

M. Blomstrom, 'The Economics of International Tax Incentives', *http://www.oecd.org/dataoecd/55/1/2487874.pdf*

Petersen et al, 'Tax Systems and Tax Harmonization in the East African Community (EAC)', p. 22, *http://www.eacgermany.org/index.php/documents-and-studies/cat_view/39-tax-harmonisation-in-the-eac/43-study-on-tax-systems-in-the-eac*

Reuters, 8 June 2011; 'AngloGold says any Tanzanian "super profits" tax will not apply'

Tanzania Export Processing Zones Authority: *http://www.epza.co.tz/About-EPZ-Program.html*

Tanzania Investment Centre at *http://www.tic.co.tz/*

The EAC Trade Report, 2009, *http://www.eac.int/statistics/index.php?option*

The Citizen, online at *http://thecitizen.co.tz/news/51-other-news/13184-fdi-inflows-into-tanzania-increase-85pc-to-hit-700m.html* (retrieved on 16th March 2012)

Uganda Investment Authority: 'Why invest in Uganda?', *http://www.ugandainvest.go.ug*

World Bank, Foreign Investment Advisory Service, Sector Study of the Effective Tax Burden in Tanzania, May 2006, *http://siteresources.worldbank.org/EXTEXPCOMNET/Resources/2463593-1213973103977/09_Tanzania.pdf*

Zanzibar Investment Policy', *http://www.zanzibarinvest.org*

ISBN 978-9987-708-06-2

policy forum

actionaid

tax justice network – Africa